epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Oktoba 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581824
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 3

### UJENZI MINARA 30 WAFARIKI MBUGANI

MAFUNDI wa Minara Tanzania (Tanzania Riggers), wameomba...



UKURASA WA 3

### LISSU AKUTANA NA WAKILI WAKE BRUSSELS

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo...



UKURASA WA 19

SAKATA LA GACHAGUA

### AMTWISHA ZIGO RUTO

NAIBU Rais Rigathi Gachagua, amejitetea mbele ya Bunge, kwa...

UKURASA 22

### POCHETTINO AANZA KUINOA MAREKANI



Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe.

# CHADEMA yajiimarisha Serikali Mitaa

UKURASA 2

## Nchimbi aagiza m/biashara Kulipwa mil. 38/-



UKURASA 5



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwataka wananchi kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mawaziri 11 wafuata wananchi mikoani

UK.2

**MICHEZO** YANGA YAJIPA NAFASI ROBO FAINALI CAF UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mawaziri watoka ofisini wafuata wananchi mikoani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NI siku 23 tangu mawaziri kuanza kukagua miradi hasa kwenye sekta nne mahsusi kwa kuangalia thamani ya fedha, kutoa maelekezo na kuzungumza na wananchi.

Mawaziri 11 wameonekana kwenye baadhi ya mikoa wakikagua miradi ya sekta ya maji, afya, elimu na barabara ambao hawawajibiki kwenye wizara zinazohusika na huduma hizo, huku katika hotuba zao wakieleza kuwa wanafanyakazi hiyo kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni mtindo unaoendana na kuhamasisha wananchi kwa maneno na kushiriki kwa vitendo, wakiwa katika mavazi ya kikazi zaidi badala ya suti.

Mawaziri na mikoa ambayo wanafanya ziara kwenye mabano ni pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (Dodoma), Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo (Lindi), Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (Mbeya).

Wengine ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi (Shinyanga), Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (Geita).

Wengine ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (Njombe), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (Mara), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax (Mtwara) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro (Kagera).

**ULEGA**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akikagua na kuzindua miradi mkoani Iringa katika shule ya sekondari Ifunda,Kiwere,Pawaga na Mboliboli amesema serikali imepeleka fedha nyingi kwenye halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule kila mahali nchini.

Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Willium Lukuvi, juzi alianza ziara ya kutembelea vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu, ikiwa ni kufafanua zaidi 4R za Rais Samia.

Kinachotafsiriwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia kwa wateule wake kutoka ofisini na kuzunguka kwa wananchi na kukagua miradi ya maendeleo.

Ni mfumo ambao hata yeye (Rais), anautumia kwa kofia zake mbili Urais na Uenyekiti wa CCM Taifa ambao kwa kiasi kikubwa tangu aingie madarakani anaufanya na kwa viongozi wake wa chama kukagua na kutoa maelekezo kwa serikali.

**MASAUNI**

Waziri Masauni akiwa mkoani Dodoma miongoni mwa miradi aliyokagua na kushiriki kuchimba msingi ni ujenzi wa vyumba vya madarasa, shule mpya ya sekondari Mnenia Halmashauri ya Kondoa Vijijini.

Akizungumza na wananchi, Masauni alisema "Si rahisi kwa Rais, Makamu na Waziri Mkuu kupita kwenye hii miradi kwenye kata zote kuona kama imekwenda kwa mujibu wa matarajio ya serikali, je, imesaidia kuondoa kero za wananchi kama serikali inavyotaka, ndio maana tumetumwa sisi kuikagua."

**JAFO**

Mkoani Lindi, Waziri Jafo alifanya ukaguzi wa miradi kwa kaulimbiu 'Rais Samia na Maendeleo Wasikie na Waone'.

Miongoni mwa miradi aliyotembelea na kuweka jiwe la msingi ni ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Chiwindi Wilaya ya Nachingwea, mradi wa maji Naipanga na mradi wa barabara Mipingo, yenye urefu wa kilometa 0.78, Wilaya ya Ruangwa inayojengwa chini ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Afya Lionja na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

**KABUDI**

Akiwa mkoani Mbeya, Waziri Kabudi aliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kukamilisha haraka ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Msingi Sama, ili kuwapunguzia kero ya kusafiri umbali mrefu kwenda shuleni.

Alisema lengo la serikali ni kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wote bila kujali hali zao huku akisisitiza kuwa elimu ni haki ya kila mtoto kwa mujibu wa sheria za nchi.

**MAVUNDE**

Waziri Mavunde ameweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa barabara ya Stendi ya Mabasi ya Kahumo yenye urefu wa kilomita moja kwa kiwango cha lami nyepesi wilayani Chato mkoani Geita na anaendelea ukaguzi huo pamoja na kuzungumza na wananchi kwenye mikutano ya hadhara.

**MKENDA**

Mkoani Njombe, Waziri Mkenda amezindua Kituo cha Afya Makoga na kuwaasa wananchi Wanging'ombe kukitunza kwa kuwa kinatoa huduma bora za afya daraja la kwanza.

**SIMBACHAWENE**

Waziri Simbachawene, aliwataka viongozi wa Mkoa wa Mara kutekeleza miradi ya maendeleo kwa usahihi ili idumu kwa muda mrefu na kutumika kikamilifu na wananchi.

Akizindua mradi wa Zahanati ya Getarungu wilayani Serengeti uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Simbachawene aliridhishwa na utekelezaji wake na kutaka halmashauri za mkoa huo kuiga utekelezaji wa namna hiyo.

**NDEJEMBI**

Waziri Ndejembi akiwa Shinyanga, alikagua mradi wa ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari Ntobo na ujenzi wa Kituo cha Afya Segesena kutoa mwezi mmoja kituo hicho kianze kufanya kazi kwa kuwa kimekamilika na kuwekewa baadhi ya vifaa tangu mwaka 2023, lakini hakijaanza huduma kwa wananchi.

**TAX**

Waziri Tax alieleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa shule za sekondari katika Manispaa ya Mtwara - Mikindani na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, na kutaka ujenzi huo uzingatie ubora na thamani ya fedha.

Mtindo huo uliwahi kutumiwa na Rais mstaafu Hayati Benjamin Mkapa wakati alipoanzisha ujenzi wa sekondari za kata.



Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akizungumza na Rais wa Hungary, Tamas Sulyok (wa pili kulia), katika Ikulu ya nchi hiyo, jijini Budapest jana. Wengine ni Mbunge wa Mexico na Rais wa Wanawake wa Umoja wa Mabunge Duniani, Cynthia López Castro (katikati) na wakalimani wa lugha. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# CHADEMA yaweka nguvu uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Jenifer Gilla**

IKIWA zimebaki siku mbili kuanza kwa uandikishwaji wa wananchi Daftari la Wakazi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema ni muhimu kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari hilo Oktoba 11 hadi 20 ili waitumie vizuri haki yao ya kuchagua viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji.

Alisema CHADEMA kimeamua kuongeza kasi ya uhamasishaji kwa sababu wameona suala hilo halijapewa uzito mkubwa wakati siku za kujiandikisha zinakaribia.

"Nimewaita kupitia kwenu kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kupiga kura ambao ni wakazi wa mtaa wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, kuanzia Oktoba 11 mpaka 20, kote nchini wanapaswa mjitokeze kwenda kujiandikisha kwa wingi," alisisitiza.

Alisema wamefanya tathmini na kuona kuwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), haifanyi jitihada za kutosha za kuhamasisha wananchi kujiandikisha kwenye Daftari la Wakazi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa zikiwa zimebaki siku mbili za uandikishaji kuanza.

Aidha, alisema hata halmashauri za wilaya zilizopewa jukumu la kusimamia uandikishaji huo kwa mujibu wa mwongozo na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hazijafanya jitihada za kutosha kuelimisha jamii kuwa zina wajibu wa kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura.

Mnyika alisema kutokuwa na elimu kunajaza imani kwa wananchi kuwa wanaweza kupiga kura kwa kutumia kadi za mpigakura walizonazo jambo ambalo sio la kweli.

"Niwaambie Watanzania wote wafahamu kuwa na kadi ya mpigakura, kuandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura lililo chini ya Tume Huru ya Taifa Uchaguzi (INEC) hakutoi uhalali wa mwananchi kupiga kura kwenye uchaguzi wa vijiji na vitongoji kama jina lako halijaingia kwenye orodha ya wapigakura inayoandikwa hivi sasa," alisema.

Alitoa rai kwa viongozi wa dini, asasi, taasisi za kiraia na vyombo vya habari kutumia wajibu wao kuhamasisha wananchi kwenda kujiandikisha, ili wapate haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi kwenye uchaguzi huo.

Alisema wanachama wa chama hicho kwa sasa wametawanyika sehemu mbalimbali wakihamasisha umma kujiandikisha, lakini jitihada za chama hicho peke yake hazitoshi kwa kuwa na wao pia wanajiandaa kwa kuweka wagombea katika uchaguzi huo.

Alitoa rai kwa wanachama wa chama hicho ha hata wasio wanachama wanaopenda demokrasia, ukweli na uadilifu kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali kupitia chama hicho kwa kuwa uchaguzi huo ni mkubwa na unahitaji wagombea wengi.

Mnyika alisema chama hicho pia kitaweka mawakala katika vituo vinavyoandikisha wapigakura ili kuhakikisha kuwa wapiga kura wasio halali hawaingizwi katika madaftari hayo na kutoa wito kwa yeyote anayetaka kushiriki kwenye uwakala ajitokeze na kuwasiliana na chama katika ngazi yoyote.

"Tukifanikiwa kulinda haki, ukweli, uhuru, demokrasia, maendeleo kupitia uandikishaji wa wapigakura safari itakuwa rahisi sana kwenye hatua nyingine zinazofuata." Alisema.

Aidha, alitoa rai kwa Watanzania wote kutoa msaada wa hali na mali kama vile maji ya kunywa kwa mawakala wa chama hicho watakaojitolea kusimamia uandikishaji huo kwa siku kumi ili haki itendeke.

# Tundu Lissu akutana na wakili wake

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amekutana na kufanya mazungumzo na mwanasheria wake, Bob Amsterdam.

Septemba 25, mwaka huu, Lissu alisema amezungumza na Amsterdam kuhusu kusudio la kufungua kesi dhidi ya kampuni ya mawasiliano ya simu ambayo inadaiwa kuvujisha mawasiliano yake ya simu, hata kufanikisha shambulio la kupigwa risasi miaka saba iliyopita.

Alifikia hatua hiyo baada ya gazeti la The Guardian la Uingereza kuripoti kesi inayoendelea mahakamani nchini humo iliyofunguliwa na aliyekuwa Ofisa Usalama wa kampuni hiyo ya mawasiliano dhidi ya kampuni mama kwa kumwachisha kazi kutokana na anachodai kufanya uchunguzi dhidi ya wafanyakazi waliovujisha taarifa hizo.

Katika ukurasa wake wa X jana, Lissu alitupia picha akiwa na Amsterdam akiandika maneno yanayosema, "Mapema leo katika mkutano wa asubuhi na Bob Amsterdam huko Steigenberger Wiltcher's Brussels."

Lissu alishambuliwa kwa risasi (inadaiwa risasi 38 zilielekezwa kwake akiwa katika gari lake) Septemba 7, 2017, kwenye eneo la nyumba za viongozi wa serikali jijini Dodoma.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari siku hiyo, Lissu alisema, "Nimewaambia walianzishe, leo (Septemba 25) nimezungumza na Bob Amsterdam, nimemwambia una mamlaka kamili ya kulianzisha. Hatujazungumza madai ya fedha, ninafikiri yatakuwa mengi sana, hatujayajadili bado."

Alisema tukio hilo katika tafsiri ya sheria, ni kitendo cha ugaidi kwa mujibu wa sheria za Tanzania; amepata ulemavu wa kudumu, hawezi kutembea sawasawa.

Alisema anatembea na risasi mgongoni na mwili umejaa vyuma kwenye goti mpaka kwenye nyonga, makovu ya risasi 16 zilizompata kati ya 38 na ya operesheni 25.

**RIPOTI YA THE GUARDIAN**

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na gazeti The Guardian la Uingereza, aliyekuwa Ofisa Usalama wa kampuni hiyo ya mawasiliano ya simu, amefungua kesi nchini humo akidai kufukuzwa kazi bila haki baada ya kupinga hatua ya kutoa data za simu za mwanasiasa Tundu Lissu mwaka 2017 na kuvujishwa bila ridhaa yake.

Anadai kuwa akiwa mfanyakazi wa kampuni hiyo, alivutiwa na mazungumzo fulani yaliyofanyika kwenye mkutano wa mtandaoni na yeye akiwa mshiriki, na kwamba alishtuka kwamba kuna jambo linaendelea pasipo yeye kushirikishwa kama mkuu wa idara.

Anadai alianzisha uchunguzi binafsi na kubaini kulikuwa na mawasiliano yasiyo ya afya baina ya kampuni na idara fulani ya serikali, ambayo yalifanyika kupitia mtandao wa WhatsApp, kampuni hiyo ya simu ikivujisha taarifa binafsi za simu za Lissu.

"Uvujishaji ulianzia tarehe 22 Agosti 2017, lakini kuanzia Agosti 29, 2017 kukawa na uvujishaji mkubwa wa taarifa za Lissu mbashara (live tracking). Taarifa hizo zilihusu maeneo aliyopo Lissu, simu zinazoingia na kutoka zikisikilizwa na SMS (ujumbe) zake zikisomwa," alidai.

# Mafundi minara 30 wafariki dunia mbugani

**Na Grace Gurisha**

MAFUNDI wa Minara Tanzania (Tanzania Riggers), wameomba kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi, kutokana na kukutana na mazingira hatarishi wanapokwenda kufanya kazi porini, mbugani na kusababisha vifo zaidi ya 30.

Pia, wameiomba serikali na kampuni zinazojihusisha na utoaji wa huduma za mawasiliano ziwape mikataba na bima za afya kwa sababu kazi wanayofanya ni ya mionzi, wanaweza kupata madhara wakati wowote na familia zao zikabaki hazina msaada.

Mwenyekiti wa Tanzania Riggers, Eliud Gobeka, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu chama hicho na mikakati ya kukiimarisha.

Alisema wamejikuta wanafanya kazi katika mazingira hayo kwa sababu shughuli zote kwa sasa zinajengwa vijijini kwenye wanyama wakali na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

"Tunakutana na hali hii kwa sababu ya kukosa vitendea kazi hatupewi magari tunatumia usafiri wa bodaboda, hivyo tunaomba kampuni zote hasa Osha, Gravity na HEC walione hili," alisema Gobeka.

Alisema mazingira hayo hatarishi yamesababisha vifo vya vijana zaidi ya 30 tangu walivyoanza kazi ya mawasiliano zaidi ya miaka 20, wanaomba wapewa fedha na mafunzo kwa wanachama hao ili kuboresha utendaji kazi wao na kuondoa tatizo hilo.

"Kazi tunazozifanya haziendeni na kipato tunachokipata, tunatamani kampuni tunazofanya nazo kazi zitambue kipato chetu na kazi tunayoifanya ni hatarishi, kwa mfano mnara wa mita 50 tunajenga kwa Sh. milioni 2.3 kiufundi hii haijakaa sawa."

"Tunaomba kampuni zote za mawasiliano, kiwango cha fedha tutakachokubaliana watulipe chote sio zitupe kianzio na ndiyo maana tunaomba mikataba ili tuweze kupata sehemu ya kuwashtaki pindi tunapopata changamoto za malipo," alisema.

Pia, alisema wameanzisha chama hicho chenye wanachama zaidi ya 500 kwa ajili ya kutetea haki zao kutokana na baadhi za kampuni kuwadhulumu fedha na kushindwa kujua waanzie wapi kuzishtaki, kwa sasa watafanya hivyo kwa sababu wameshasajili chama hicho.

Katibu wa chama hicho, Baraka Urio, aliiomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwawezesha vijana kupata mafunzo na vifaa vya kufanyia kazi ili kuleta ufanisi katika kazi zao.

Alisema baadhi ya kazi wanazofanya ni kujenga minara mipya, nguzo za umeme, kusafisha vioo kwenye majengo marefu, kujenga magodauni marefu na kuchomelea.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
09.10.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumapili tarehe 13-10-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Dar es Salaam Port** kupitia Mlandizi gari hizo zina namba za usajili:

**T 959 DTN / T 243 AGZ**
**T 998 EDR / T 874 BTU**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20.00**
**Upana - mita 4.30**
**Kimo - mita 4.80**

2. Njia zitakazotumika: **Mzenga kupitia Mlandizi** hadi **Dar Es-Salaam** gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



*FORM NO. A/1*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**
**RM REFERENCE NO. 2024409061000022197, CASE NO 22197/2024**
**BETWEEN**
**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD......................................PLAINTIFF**
**AND**
**VISION SCOPE LIMITED........................................................DEFENDANT**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**

**(O. V, r 1 CPC)**

To: **MANAGING DIRECTOR**
**VISION SCOPE LIMITED**
**SINZA A AREA, ALONG SAM NUJOMA ROAD**
**OPPOSITE MLIMANI CITY MALL, KINONDONI MUNICIPALITY**

**WHEREAS** the above-named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within **twenty-one (21)** days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon. **RAHIM MUSHI** Resident Magistrate on the 08... **day of** ...November..... **2024** at 8.30am.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this 27...... **day of** ...Sept........, **2024**

......................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**KISUTU – DAR ES SALAAM**

I **HEREBY** acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this ........................day of........................, 20...............

......................................
**DEFENDANT**



*FORM NO. A/1*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**
**RM REFERENCE NO. 2024409061000022198, CASE NO 22198/2024**
**BETWEEN**
**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD......................................PLAINTIFF**
**AND**
**SAMNA (T) INVESTMENTS LIMITED....................................DEFENDANT**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**

**(O. V, r 1 CPC)**

To: **MANAGING DIRECTOR**
**SAMNA (T) INVESTMENTS LIMITED**
**MAARIFA HOUSE, OPPOSITE THE ATC HOUSE**
**OHIO STREET, ILALA MUNICIPALITY**

**WHEREAS** the above-named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within **twenty-one (21)** days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon. **RAHIM MUSHI** Resident Magistrate on the 08... **day of** November... **2024** at 8.30am.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this 27.. **day of** Sept..., **2024**

......................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**KISUTU – DAR ES SALAAM**

I **HEREBY** acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this ........................day of........................, 20...............

......................................
**DEFENDANT**

HABARI PICHANI

# MATUKIO KATIKA PICHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA




Wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania, wakifanya matembezi ya amani kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja 2024, kutoka Makao Makuu ya benki hiyo, Exim Tower mpaka tawi lake la Samora Avenue, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA ZOTE: WAPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa pili kushoto), akiwaongoza Mkuu wa Uendeshaji NBC, Alelio Lowassa (kulia) na wateja waliohudumiwa na benki hiyo kwa zaidi ya miaka 30 akiwamo, Zuhura Maganga (kushoto) na Asaa Simba (wa pili kulia), kukata keki maalum ikiwa ni ishara ya kuzindua maadhimisho ya Mwezi wa Huduma kwa Wateja, jijini Dar es Salaam juzi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), akiwa pamoja na viongozi waandamizi wa benki hiyo, na baadhi ya wateja, wakishuhudia uzinduzi wa mfumo mpya wa kidijitali wa huduma kwa wateja unaotumia teknolojia ya akili mnemba (AI), iliyopewa jina la 'Elle', wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja 2024, jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Azania Tawi la Geita, Rhoda Baluhya, wakati alipotembelea Maonesho ya Saba ya Teknolojia ya Madini, mjini Geita jana.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), akimwangalia mtoa huduma za kidigitali wakati wa uzinduzi wa huduma ya NMB Jirani, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara Benki hiyo, Filbert Mponzi na kulia ni Ofisa Mkuu wa Teknolojia na Mabadiliko ya Kidijitali wa NMB, Kwame Makundi.

## HABARI KITAIFA

# Nchimbi aagiza m'biashara kulipwa madai ya miaka 12

**Na Halfani Chusi,** MEATU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi, Dk. Emmanuel Nchimbi, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Meatu, mkoani Simiyu kumlipa mfanyabiashara ndani ya mwezi huu madai yake ya Sh. milioni 38 alizosotea kwa miaka 12.

Mfanyabiashara huyo alimlalamikia Dk. Nchimbi akiwa katika mkutano wa hadhara wilayani Meatu, mkoani Simiyu, akidai fedha hizo tangu mwaka 2012, lakini mpaka sasa hajalipwa licha ya kuwa na nyaraka zote.

Baada ya Dk. Nchimbi kusikiliza lalamiko lake aliagiza halmashauri hiyo imlipe haraka iwezekanavyo.

"Huyu aliyelalamika mbele yangu mwezi huu usiishe, alipwe fedha zake na ninakupa namba yangu ili usipolipwa uniambie," alisema Nchimbi huku akishangiliwa na wana-Meatu.

Awali, Dk. Nchimbi alizitaka taasisi za serikali na halmashauri nchini kutotangaza zabuni ikiwa hawana bajeti ili kuiepusha serikali na mzigo wa madeni.

Pia, alikemea baadhi ya viongozi serikalini kutanguliza mbele maslahi yao binafsi na kwamba wapo baadhi ya viongozi ambao wakipata nafasi wanaanza kutanguliza mbele familia zao.

Kutokana na hali hiyo, alisema CCM itaendelea kushirikiana na serikali kupambana na wanaohujumu miradi na kazi nzuri zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, alisema timu yake ya kuangalia kero imeongea na wananchi 48 ambao wamewasilisha kero 89 ambazo zimekabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa (Kenani Kihongosi) na ofisi yake imechukua namba za simu kwa ajili ya kuwasiliana nao kuona kama wamesaidiwa.

Kuhusu kero iliyowasilishwa na mmoja wa wakazi kuhusu Shule ya Msingi Mwangudo kutokamilika kwa wakati, Nchimbi alimwita Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Faudhia Ngatumbara ambaye alifafanua kwa kusema:

"Jitihada za ujenzi zinaendelea na matarajio yao mpaka kufikia Januari mwakani itakuwa tayari imeanza kupokea wanafunzi," alisema.

Nchimbi aliahidi ofisi yake itachangia Sh. 10,000,000 kuhakikisha shule hiyo inakamilika kwa wakati.

Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amosi Makalla, alisema hawatasimamisha wagombea wenye makandokando katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

"Niwahakikishie CCM itawaletea wagombea safi wanaokubalika kufanyakazi na wananchi, hivyo muwapigie kura wagombea wa CCM.

"Hatutadiriki hata kidogo kuwaletea watu ambao wanamkandokando na sisi hatuna haja ya kusimamisha wagombea ambao tutahangaika kuwasafisha kwa dodoki, hivyo tutawaletea watu safi."

Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, alisema zawadi ya serikali kwa wananchi wa Meatu ni kujenga vituo viwili vya zana za kilimo ambayo kila kimoja kitakuwa na trekta 20.

Alisema kupitia vituo hivyo mwananchi atalima kwa kutumia trekta hizo kwa gharama ya Sh. 40,000 kwa ekari ingawa serikali ina mpango wa kushusha zaidi kiwango hicho.

**CHADEMA**

Katika mkutano uliofanyika eneo la Luguru wilayani Itilima Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Meatu, Terry Kilugala, Katibu wake Gershon Mipawa pamoja na wanachama wao zaidi ya 60 walihamia CCM na kupokewa na Nchimbi.

Akizungumza baada ya kupokewa Kilugala, alisema wameshawishika kutokana na utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tulikuwa tunaenda Mwanza siku mbili kwa ubovu wa barabara, leo tunaenda na kurudi. Lazima tuseme ukweli, CCM imefanya kazi.

Balozi Nchimbi, akiwapokea, alisema: "Hawa ndugu zetu wameona mbali mapema, maana viongozi wakubwa kama Peter Msigwa kaona shida zao, wewe unasubiri nini? Rudini CCM, na nawapongeza wote mliojiunga na CCM, viongozi pamoja na wanachama. Karibuni sana tufanye kazi ya kujenga taifa pamoja."

Kadhalika, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kushiriki uchaguzi ili waweze kupata nafasi ya kuchagua viongozi wa chama hicho akitamba ndio wana uwezo na maarifa ya kuongoza nchi.

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
THE CITY COUNCIL OF DODOMA
CCD

## TANGAZO LA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KITALU "DA" NA "N"

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE AMBAO HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA UNUNUZI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KATIKA KITALU "DA" NA "N" KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE 3 HADI 16 OKTOBA, 2024.

KUSHINDWA KUKAMILISHA MALIPO HAYO; KIWANJA HICHO KITATOLEWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA TAARIFA ZAIDI KWAKO NA WEWE UTAREJESHEWA FEDHA YAKO BAADA YA KUKATWA ASILIMIA 10 KWA GHARAMA ZA USUMBUFU.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA**

*FORM NO. A/1*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**
**RM REFERENCE NO. 2024409061000022196, CASE NO 22196/2024**
**BETWEEN**
**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD.......................................PLAINTIFF**
**AND**
**SAMCAT (T) LIMITED............................................................DEFENDANT**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**

**(O. V, r 1 CPC)**

To: **MANAGING DIRECTOR**
**SAMCAT (T) LIMITED**
**PLOT NO. 2136, BLOCK E, GOBA AREA**
**UBUNGO MUNICIPALITY**

**WHEREAS** the above-named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within **twenty-one (21)** days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon. **RAHIM MUSHI** Resident Magistrate on the 08... **day of** ...November....... **2024** at **8.30am.**

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this ...27...... **day of** ...Sept........, **2024**

........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**KISUTU – DAR ES SALAAM**

I **HEREBY** acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this .......................day of......................., 20..............

........................................
**DEFENDANT**

*FORM NO. A/1*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**
**RM REFERENCE NO. 2024409061000022143, CASE NO 22143/2024**
**BETWEEN**
**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD.......................................PLAINTIFF**
**AND**
**BAGENZI ASSOCIATES CO. LIMITED....................................DEFENDANT**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**

**(O. V, r 1 CPC)**

To: **MANAGING DIRECTOR**
**BAGENZI ASSOCIATES COMPANY LIMITED**
**SINZA AREA, SINZA ROAD STREET, KINONDONI MUNICIPALITY**

**WHEREAS** the above-named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within **twenty-one (21)** days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon. **RAHIM MUSHI** Resident Magistrate on the 08...**day of** ..November.... **2024** at 8.30am.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this ..27... **day of** Sept...., **2024**

........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**KISUTU – DAR ES SALAAM**

I HEREBY acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this .......................day of......................., 20..............

........................................
**DEFENDANT**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wiki ya Huduma kwa Wateja itoe funzo

**TAASISI** mbalimbali nchini na duniani kwa ujumla zinaadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja. Katika kuadhimisha wiki hii, taasisi mbalimbali zinaonesha shughuli mbalimbali kuwahudumia wateja katika maeneo mbalimbali pamoja na kutoa elimu kuhusu huduma na kazi zinazofanya.

Katika kuonesha umuhimu wa Wiki ya Huduma kwa Wateja, wakuu wa taasisi wakiongozwa na maofisa watendaji wakuu, wakurugenzi, mameneja na maofisa wote mpaka wafanyakazi wa ngazi za chini, wako mstari wa mbele kuwahudumia wateja na kuwaeleza shughuli na huduma zinazotolewa katika kampuni na mashirika hayo.

Mara nyingi, wakati wa kuadhimisha wiki hii, imeshuhudiwa wakurugenzi watendaji wa benki, mathalan, wakiwa kwenye madirisha ya kutoa huduma. Yote hiyo ni kuonyesha umuhimu wa huduma kwa wateja, ikiwa pia njia ya kushawishi wale wasiotumia huduma au bidhaa zao kujiunga na taasisi hizo ili kunufaisha pande zote.

Wakati wiki hii ikiadhimishwa, kumekuwa na maalamiko kwa baadhi ya wateja na wadau kuwa zimo taasisi ambazo zinasherehekea wakati huduma zake ni za viwango duni au kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma. Moja ya taasisi hizo ni za huduma za maji.

Moja ya taasisi hizo imewatakia wateja wake maadhimisho mema ya wiki ya maji na wateja kutoa maoni mbalimbali kwenye makundi sogozi wakihoji viongozi na watumishi wa taasisi hiyo wanajisikiaje wanapoadhimisha wiki hii adhimu wakati wananchi wanalalamikia kukosa maji?

Kutokana na hoja hiyo, viongozi wa serikali wenye dhamana katika sekta hiyo na watendaji wa mamlaka wameibuka na kutoa ufafanuzi kuwa kuna kasoro za kifundi na zingine ziko nje ya uwezo wao katika kuwafikia wateja, hivyo kuomba radhi kwa wale wanaokwazwa na hali hiyo. Kwa kutoa maelezo hayo, wamedhihirisha ule msemo kwamba muungwana ni kitendo.

Wiki ya Huduma kwa Wateja huadhimishwa kila mwaka kwa taasisi kufanya mambo mbalimbali. Kwa taasisi zilizo makini, hutumia maadhimisho hayo kufanya tathmini ya mafanikio, kasoro na upungufu katika utoaji wa huduma.

Pale penye mafanikio, hupongezana na pia kuangalia ni namna gani ya kuongeza viwango katika utoaji wa huduma ili kuvutia wateja zaidi.

Aidha, pale panapojitokeza kasoro au kutofikiwa malengo yaliyokusudiwa, hujiuliza sababu na kuchukua hatua stahiki ili kuziondoa na hatimaye kuboresha viwango vya huduma.

Miongoni mwa maeneo ambayo yamekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wateja, ni huduma mbovu ikiwamo lugha mbaya kwa wateja, kutokuwapo mazingira rafiki ya utoa huduma na viwango vinavyotolewa kuwa vya hali ya chini.

Katika hoteli kwa mfano, imekuwa ikielezwa kuwa huduma zinazotolewa katika tasnia hiyo ni za viwango vya duni hatua ambayo huwakimbiza wateja wengi. Mteja tangu kuingia, hukaribishwa isivyostahili na hiyo imesababisha hoteli nyingi kuanzishwa kwa kishindo na kuporomoka viwango na hatimaye kufungwa kwa muda mfupi.

Hata katika baadhi ya hospitali, kumekuwa na malalamiko kuwa huduma zinazotolewa si rafiki kwa wagonjwa. Baadhi ya wauguzi, kwa mfano, wamekuwa wakidaiwa kutoa lugha chafu kwa wagonjwa au kutoa huduma kwa kusuasua jambo ambalo wakati mwingine husababisha vifo ambavyo vinaweza kuzuilika.

Kwa jumla, Wiki ya Huduma kwa Wateja ya mwaka huu, itoa fundisho kwa taasisi kujipanga upya katika utoaji huduma ili kupaa katika viwango vyao badala ya kufanyika kila mwaka kwa mazoea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanufaika mikopo asilimia 10 inaanza

Na Beatrice Moses

**MANISPAA** kadhaa zimetoa matangazo kuhusu kurejeshwa tena kwa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Hii ni taarifa njema kwa makundi hayo ambayo kwa muda sasa mikopo hiyo ilisimama ili kuandaliwa utaratibu bora.

Ikumbukwe fedha hizo ni zile zinazoleta unafuu kutokana na masharti yake hasa ikilinganishwa na mingine hasa inayotolewa na baadhi ya taasisi binafsi.

Kwa kuwa licha ya kuwa na masharti magumu imetajwa kusababisha baadhi ya wateja kuwa na hali ngumu, kwa kubambikiwa riba.

Hali ngumu hiyo iwakumbushe wanufaika kadhia inayosababisha mikopo hiyo kuitwa kausha damu'.

Ni kwa sababu watu wamelazimika kukimbia familia kutokana na riba kubwa walizotozwa na hata wengine kufilisika.

Tangazo la Manispaa ya Ubungo linabainisha kuwa Sh. bilioni 3.5 zimetengwa kwa ajili ya mkopo huo, na kwamba vikundi ambavyo vinadaiwa fedha za nyuma havitakopeshwa.

Hili ni angalizo muhimu kwa kuwa wasiorejesha mikopo hiyo nafuu kwa wakati wamechelewesha au kukwamisha mzunguko wa mkopo huo kwenda inavyotakiwa.

Ni kulingana na kanuni zilizowekwa ili kufanikisha kuwainua kimtaji na kimapato wajasiriamani katika makundi hayo.

Kwa mujibu wa kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019, husasan unaangalizo kwa warejeshaji mikopo.

Zinabainisha kuwa kikundi kitahesabika kuwa kimepoteza sifa ya kupata mkopo endapo, hakijamaliza kurejesha mkopo uliotolewa awali, au kimetoa taarifa za uongo kwa mamlaka za serikali za mitaa ili kupata mkopo.

Ikibainika kimetumia fedha za mkopo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoombewa bila idhini ya mamlaka ya serikali ya mtaa au kimeshindwa kurejesha mkopo.

Kuhusu kutoa mikopo imebainishwa kuwa Mkurugenzi wa Manispaa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha wilaya inatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo hiyo.

Aidha, mikopo inatolewa kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizo na kwamba vikundi vilivyokopeshwa vinarejesha mikopo kwa wakati.

Kadhalika, inabainisha kuwa mgao wa fedha za mikopo unapaswa kufanywa kwa kuzingatia masharti ya kanuni na itatolewa kwa kuzingatia mgawo wa kiasilimia.

Vikundi vya vijana, wanawake na wenye mahitaji maalumu.

Jambo lenye neema ni kwamba mikopo itakayotolewa chini ya kanuni hizo haitotozwa riba.

Wakati sifa za kupata mkopo zinabainishwa kuwa kikundi cha wanawake, vijana au watu wenye ulemavu kitakuwa na sifa ya kupata mkopo endapo, kimesajiliwa.

Kanuni zinabainisha kuwa kikundi kinapaswa kujishughulisha na ujasiriamali au kinakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati.

Kwa kikundi cha wanawake au vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia 10 na kuendelea na kwa wenye mahitaji maalumu idadi ya wanakikundi isipungue watano na isiyozidi 10.

Pia kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi na wanachama wake ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri zaidi ya miaka 18.

Naamini kwamba serikali za mitaa pamoja na kuwa wametingwa na maandalizi ya uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu, bado wataona umuhimu wa kuwajibika kwa wanufaika kuhusu mikopo.

Ni kwa kutoa tangazo kwa umma kwa madhumuni ya kuutarifu na vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuhusu fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo yao.

# MATANGAZO


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MPANGO WA UREJESHAJI STAHILI ZA WAGUSWA WA BOMBA LA MAFUTA: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUENDELEZA UFUGAJI BORA WA NYUKI. NA: REQ 00000620**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") inaalika kampuni au mashirika yenye uzoefu na sifa nzuri kuleta maombi yakuonyesha nia yao ya kubuni na kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Nyuki kwa kaya zilizoathiriwa na mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini ya ardhi linalovuka mipaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, likipitia katika mikoa nane – Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

EACOP inatekeleza mipango ya urejeshaji wa maisha kwa Kaya zilizoathiriwa na Mradi (PAHs). Mradi wa EACOP uko mbioni kuanza utekelezaji wa Mpango wa Ufugaji Nyuki ulioboreshwa kwa kaya za waguswa takribani katika wilaya 10 ambapo shughuli za ufugaji nyuki zinafaa. Ubunifu wa mpango huu uko katika hatua za mwisho na huenda ukajumuisha lakini hauishii katika:

- Ushirikishwaji wa kaya ili kuthibitisha uwezo wao wa kuwa sehemu ya mpango.
- Uainishaji wa kaya kulingana na miundo ya mpango.
- Mafunzo juu ya uzalishaji wa mizinga ya nyuki ya kisasa iliyo boreshwa.
- Utafutaji na usambazaji wa vifaa vya ufugaji nyuki na mavazi ya kujikinga yanayofaa kwa nyuki wa Tanzania.
- Mafunzo na kujenga uwezo wa kaya juu ya masuala yote muhimu ya ufugaji nyuki, ikijumuisha mafunzo ya awali na ya juu ya ufugaji nyuki, aina za mizinga zinazopendekezwa, muundo na ukarabati wa mizinga, vifaa vinavyohitajika, uwekaji bora wa mizinga, na mbinu bora za kukusanya, kuchakata na kuvuna asali.
- Msaada katika kuandaa kalenda za msimu wa uzalishaji wa asali.
- Kuanzisha uhusiano na sekta binafsi kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa masoko na uwezekano wa uwekezaji katika uzalishaji wa asali katika wilaya zilizoathiriwa na Mradi.
- Kusaidia upatikanaji wa fursa za kuongeza thamani ya mazao ya Nyuki.
- Huduma za ughani kwa kaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Mashirika yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, uzoefu kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au amekwisha tuma maombi yaliyoidhinishwa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **28/10/2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **EOI 000000620: Maombi ya kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Nyuki.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MPANGO WA UREJESHAJI STAHILI ZA WAGUSWA WA BOMBA LA MAFUTA: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUENDELEZA UFUGAJI BORA WA KUKU. NA: REQ: 00000618**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") inaalika kampuni au mashirika yenye uzoefu na sifa nzuri kuleta maombi yakuonyesha nia yao ya kubuni na kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa kuku kwa kaya zilizoathiriwa na mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini ya ardhi linalovuka mipaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, likipitia katika mikoa nane – Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

EACOP inatekeleza mipango ya urejeshaji wa maisha kwa kaya zilizoathiriwa na Mradi. EACOP iko mbioni kuanza utekelezaji wa Mpango wa ufugaji bora wa Kuku kwa kaya za waguswa katika mikoa yote minane ambako mradi unatekelezwa. Uandaaji wa mpango huu uko katika hatua za mwisho na huenda ukajumuisha lakini hauishii katika:

- Ushirikishwaji wa kaya ili kuthibitisha uwezo wao wa kuwa sehemu ya mpango.
- Uainishaji wa kaya kulingana na miundo tofauti ya mpango.
- Mafunzo na ujenzi wa uwezo wa kaya katika masuala yote ya uzalishaji na usimamizi wa kuku.
- Mafunzo ya kujengea kaya uwezo wa kuanzisha na kuendesha biashara ya ufugaji kuku ili kuongeza kipato cha kaya husika.
- Mafunzo ya watoa huduma za ughani katika sekta ya mifugo kwa jamii.
- Ununuzi na usambazaji wa vifaranga vya Kuku (aina za kienyeji na zilizoboreshwa zinazofaa katika mazingira husika mazingira)
- Utoaji wa chakula cha kuku kwa waguswa kwa kipindi kifupi, ikifuatiwa na mafunzo ya uzalishaji chakula cha kuku.
- Kutambua na kushirikiana na wauzaji wa pembejeo za mifugo ili kutoa na kusambaza vifaa muhimu vya mifugo, ikiwa ni pamoja na chanjo, dawa na virutubisho.
- Kusaidia kaya kujenga mabanda endelevu ya kuku.
- Huduma za ughani kwa kaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Mashirika yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, uzoefu kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ame kwisha tuma maombi yaliyoidhinishwa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **3/11/2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **EOI 0000618 Maombi ya kutekeleza mpango wa ufugaji bora wa kuku.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

**HABARI KITAIFA**

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MPANGO WA UREJESHAJI STAHILI ZA WAGUSWA WA BOMBA LA MAFUTA: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUENDELEZA UFUGAJI BORA WA WANYAMA. NA: REQ 00000619**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") inaalika kampuni au mashirika yenye uzoefu na sifa nzuri kuleta maombi yakuonyesha nia yao ya kubuni na kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Wanyama kwa kaya zilizoathiriwa na mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini ya ardhi linalovuka mipaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, likipitia katika mikoa nane – Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

EACOP inatekeleza mipango ya urejeshaji wa maisha kwa kaya zilizoathiriwa na Mradi. EACOP iko mbioni kuanza utekelezaji wa Mpango wa kuendeleza ufugaji bora wa Wanyama kwa waguswa katika mikoa minne ambako utekelezaji wa mradi wa EACOP unafanyika. Uandaaji wa mpango huu uko katika hatua za mwisho na huenda ukajumuisha lakini hauishii katika:

- Ushirikishwaji wa kaya ili kuthibitisha uwezo wao wa kuwa sehemu ya mpango.
- Uainishaji wa kaya kulingana na miundo tofauti ya mpango.
- Mafunzo na kuzijengea kaya uwezo katikamasuala yote muhimu katika uzalishaji na usimamizi bora wa mifugo na wanyama wadogo wadogo wa kufugwa.
- Mafunzo kwa watoa huduma za ughani za mifugo katika jamii.
- Kuandaa na kutoa mafunzo juu ya kalenda za usimamizi wa mifugo.
- Kusaidia kuanzisha vituo vya wafugaji wa mifugo.
- Kusaidia uanzishaji na uendelezaji wa vyama au ushirika wa wafugaji.
- Kukarabati mabwawa ya kuogesha mifugo.
- Kuunganisha kaya zilizoathiriwa na Mradi (PAHs) na sekta binafsi kwa ajili ya kupata mbegu bora za mifugo kwa kukodisha ng'ombe wa nyama na maziwa.
- Kutoa ushauri na kusaidia upatikanaji wa fursa za kuongeza thamani ya mazao ya mifugo.
- Kutoa huduma za ughani kwa kaya za waguswa kwa kipindi cha miezi 18-24.

**VIGEZO MUHIMU:**

**Mashirika yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, uzoefu kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au amekwisha tuma maombi yaliyoidhinishwa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **30/10/2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **EOI 00000619 Mpango wa ufugaji bora wa Wanyama**. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni au kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

# Wajasiriamali wahimizwa kusajili biashara BRELA

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAJASIRIAMALI wadogo nchini wamehimizwa kusajili biashara zao kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kuwa na nafasi ya kupata mikopo kwenye benki, tenda ndogondogo na kubwa za biashara na kujipambanua kiushindani kwenye soko la bidhaa.

Ofisa Leseni Mkuu kutoka BRELA, Abas Kotema, alisema juzi kuwa wajasiriamali wanayo nafasi kubwa ya kukuza biashara zao kwa kupata mikopo kupitia benki hasa pale wanaposajili biashara zao na kuwa zenye kutambulika.

Alisema usajili wa majina ya biashara upo wa aina kuu tatu ikiwamo wanaomiliki mtu mmoja ambao humtambulisha mjasiriamali sokoni kulingana na biashara aliyonayo, kupata mitaji kupitia mikopo kwenye benki, kuingia mikataba mbalimbali na kupata tenda ndogo na za serikali.

Aidha, Kotema alifafanua kuwa pia kuna usajili wa jina la biashara linalomilikiwa na watu wawili hadi 20 na kuwa tayari wamerasimisha biashara yao na kuwa na nafasi ya kupata huduma kama au zaidi ya umiliki wa mtu mmoja.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara kutambua kuwa kurasimisha biashara na kumiliki nembo za biashara kupitia BRELA kutawasaidia kuepuka kufikishwa mahakamani kisheria kwa kutumia nembo ya mtu mwingine.

"Lakini pia tunatoa leseni za biashara kundi A, kwa mujibu wa sheria ya leseni ya mwaka 1972 namba 25 ni kwamba leseni zipo katika makundi maalum za kundi A zinazotolewa na BRELA chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara zenye sura ya kitaifa na kimataifa, humwezesha mjasiriamali kuingiza au kutoa biashara nje ya nchi, leseni za kundi B hutolewa na halmashauri husika ambazo hazitumiwi kwenye halmashauri nyigine," alisema.

Hata hivyo, aliwahimiza wenye kampuni ambao wamesajili biashara kabla ya BRELA haijaanza, kutoa huduma kwa njia ya mfumo kuhamasika kupata elimu na kuingizwa kwenye mfumo huku wakiwa wamesamehewa tozo zilizoongezeka.

Kotema alisema tangu mwaka 2018 mwezi Aprili, BRELA ilianza kutumia mfumo katika utoaji huduma na msamaha huo utakuwa wa mwaka mmoja kuanzia mwezi Mei, mwaka huu hadi mwezi Mei 2025, ukihusisha wenye kampuni walioingia BRELA miaka iliyopita ambao bado hawajaingizwa kwenye mfumo. "Kwanza tumetoa msamaha kwa tozo na faini kwa kampuni ambazo zinatakiwa kuwekewa mizania ya mwaka na BRELA ambayo inatakiwa kulipwa Sh. 22,000 na ukichelewa kuna nyongeza ya asilimia tano, kwa hiyo tumetoa msamaha kwa kampuni na kulipa nusu ya deni analodaiwa," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kupata leseni ya kuzalisha umemekutoka kwa kampuni ya Mtibwa Sugar Estate Ltd . EWURA inakaribisha maoni au pingamizi dhidi ya maombi hayo. Taarifa za mwombaji, mitambona aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:-

| Na. | MAELEZO |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | Mtibwa Sugar Estate Ltd.<br>S.L.P. 42, Mvomero, Morogoro. |
| **Mahali ulipo Mtambo** | Kiwanja Na. 194/1, Turiani – Mtibwa, Morogoro. |
| **Taarifa za Wanahisa** | 1. Nassoro Ally Seif S.L.P. 16541, Dar es Salaam, **50%**<br>2. Seif Ally Seif S.L.P. 16541, Dar es Salaam, **50%** |
| **Maelezo ya Mtambo** | Mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati (MW) kumi na tano (15) MW kwa kutumia nishati inayotokana na tungamotaka. Umeme utakaozalishwa utatumiwa na mwombaji mwenyewe. |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa muda wa miaka mitano (5) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu atakayewasilisha maombi kwa maandishi.

Imetolewa na:-
**Mkurugenzi Mkuu**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga (wa tatu kushoto), akiongoza hafla ya kukabidhi jiko la gesi kwa mwalimu kutoka jijini Arusha mwishoni mwa wiki, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani yaliyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, Mrisho Gambo (wa pili kulia), kwa kushirikiana na wadau ikiwamo Benki ya Exim, iliyotoa majiko 1,000. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Teknolojia yaleta neema kwa wakulima wa mboga

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TEKNOLOJIA ya kilimo ya kuvuta na kusukuma wadudu imeanza kuonyesha matokeo chanya kwa wakulima wadogo wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro kudhibiti wadudu waharibifu na madhara ya kemikali sumu kwa walaji wa mboga na matunda nchini.

Shirika la World Vegetable Center, linalotekeleza Mradi wa Fresh katika mashamba darasa ya Masaera wa wilaya hiyo, linalenga kuwasaidia wakulima wadogo wa kabichi, nyanya na vitunguu

kuongeza kipato na kuimarisha lishe nchini kwa kutumia teknolojia hiyo ijulikanayo kama 'Push Pull Technology'.

Akizungumza jana na wakulima 100 waliokuwa wakipatiwa elimu kuhusiana na teknolojia hiyo, Mtaalamu wa Kilimo Biashara wa World Vegetable Center, Judith Assenga, alisema imewasaidia wakulima kupunguza matumizi ya dawa na kudhibiti wadudu waharibifu wakiwamo kimamba na funza.

"Kwa kutumia teknolojia hii inayofundishwa hapa kupitia Mradi wa Fresh, wakulima wetu watalima sasa mazao bila ya kutumia sumu," alisema na kuongeza kuwa:

"Wakulima katika kudhibiti hao wadudu wanatumia sana dawa kama vile penetrecer, ukiangalia mwisho wa siku ni gharama sana kwa mkulima."

**Akiwa katika shamba darasa la Kijiji cha Masaera, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Hamza Mwinyihija, alisema teknolojia ya push pull waliyoanza kuitumia wakulima hao kuna mazao**

Akizungumzia kuhusu afya ya mkulima anayepiga dawa kwenye mimea yake, alisema inakuwa hatarini kutokana na kutovaa vifaa vya kujikinga.

Akiwa katika shamba darasa la Kijiji cha Masaera, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Hamza Mwinyihija, alisema teknolojia ya push pull waliyoanza kuitumia wakulima hao kuna mazao ambayo yanavuta na kusukuma.

"Kwa mfano katika majaribio yetu tuliyoyafanya, kabichi ndio zao ambalo tunaliangalia; na mazao mengine ni kama kitungu, mgagani na maharage, ambayo ni mahususi kwa kuvuta wadudu wa kabichi.

Kwa hiyo teknolojia hii ni nzuri kwa sababu matumizi ya sumu au viuatilifu imekuwa changamoto kubwa sana, wakulima hawawezi kulima bila ya kutumia sumu. Unakuta sasa zile sumu zinasababisha madhara makubwa sana kama magonjwa ya saratani na shinikizo la damu."

Prosper Tira, mkulima, Mkazi wa Kijiji cha Masaera, akielezea umuhimu wa teknolojia hiyo, alisema inawasaidia wakulima wa mboga. "Faida ya kwanza ni kuotesha mazao mengi sehemu moja ambayo yanakinzana. Inapunguza matumizi ya sumu ambayo si ya lazima. Teknolojia hii ikisambazwa kwa wakulima wengine itatunufaisha na walaji. Hii teknolojia isambazwe kwa kila mkulima nchini wa mazao ya mboga ili kupunguza athari za kemikali kwenye chakula," alisema Tira.

# 'Huduma za uchunguzi, upimaji saratani zisogezwe haraka Mwanga'

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

SERIKALI imeelekeza kusogezwa haraka huduma za uchunguzi wa magonjwa na upimaji wa saratani ya matiti wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro ili kuokoa maisha ya wanawake na wajawazito.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alitoa maelekezo hayo jana baada ya kukagua ujenzi wa Mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Mwanga, unaotekelezwa kwa fedha za serikali.

"Kwa sasa, mgonjwa akitakiwa kupata huduma za X-Ray anakwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawezi au Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, umbali mrefu wa kilometa zaidi ya 50.

Sasa ili kuepusha hizo gharama, naelekeza kuanzia sasa huduma hizo zitatolewa katika Wilaya ya Mwanga. Huduma hizi zitasaidia kuokoa gharama za wananchi wetu wa Mwanga, kwenda kutunza mgonjwa wao mbali, na zitasaidia kuokoa uchumi wetu.

...Maana mtu badala ya kuwaza mambo ya kuongeza uchumi, anawaza mgonjwa wake yupo KCMC, Rais wetu (Samia Suluhu Hassan) amesema hapana inatosha; hayo yote yafanyike wapi? anataka hapa hapa Mwanga."

Kwa mujibu wa Waziri Mhagama, Rais Samia, ameelekeza kutolewa kwa Sh. bilioni mbili kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo ya Wilaya ya Mwanga na Sh. milioni 500 ununuzi wa vifaa tiba.

Alitaja miongoni mwa vifaa vitakavyonunuliwa katika hospitali hiyo kuwa ni mashine ya kupima saratani ya matiti kwa wanawake, Ultrasound wajawazito na dawa.

"Nimeingia kwenye jengo la mionzi, nimekuta digital X-Ray toleo la kisasa, ina uwezo wa kugeuza mwili wa mgonjwa na kupiga picha kwa ajili ya uchunguzi, haya mlikuwa mnayaona wapi ndugu zangu? " alihoji.

# Uzalishaji kahawa washuka Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UZALISHAJI wa kahawa Mkoa wa Kilimanjaro, umepungua hadi kufika wastani wa tani 6,000 kwa mwaka kutokana na changamoto mbalimbali, imefahamika.

Serikali ya mkoa huo imetaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni kubadilishwa matumizi ya ardhi ya kilimo cha zao hilo na kupandwa mazao ya mboga na nyanya. Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu ameagiza Bodi ya Kahawa nchini (TCB) kuhamasisha wadau wa zao hilo kutumia fursa ya makubaliano kwenye eneo Huru la Biashara Afrika (AfCTA) ili kukuza biashara ya zao hilo ya Tanzania katika nchi za Afrika na kuondoa utegemezi wa soko la nchi za Ulaya na Japan.

Alikuwa akizungumza jana mjini hapa wakati uzinduzi wa tamasha la kahawa kwa mwaka huu lililoandaliwa na TCB kwa kushirikiana na wadau wa zao hilo nchini. "Kwa sasa uzalishaji wetu umepungua hadi kufika wastani wa tani 6,000 kwa mwaka, kitu ambacho si kizuri kwa maendeleo ya mkoa wetu. Pamoja na umaarufu wa kahawa kote duniani, unywaji wa kahawa nchini unakuwa kwa kasi ndogo," alisema.

Kwa mujibu wa Babu, takwimu alizonazo mpaka sasa, unywaji wa kahawa ni asilimia saba tu ya kahawa yote inayozalishwa nchini.

"Unywaji huu mdogo unachangiwa na sababu kadhaa, zikiwamo imani potofu na matatizo ya kiafya, hivyo kusababisha watu wengi kuogopa kutumia kinywaji hiki tofauti na uhalisia.

...Hivyo ni vyema tukatumia fursa hii kutafakari changamoto zinazopelekea kushuka kwa uzalishaji na kuja na suluhu zinazotekelezeka za kurudisha zao la kahawa katika mkoa wetu."

Alizitaja baadhi ya changamoto wadau wa kahawa nchini wanatakiwa kuzitafakari na kuzipatia majibu kuwa ni mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha kupungua kwa maji kwa ajili ya umwagiliaji, mtawanyiko mbaya wa mvua na matumizi duni ya pembejeo hususani mbolea za viwandani hasa kwa wakulima wadogo.

Nyingine ni tija ndogo ya uzalishaji na kuyumba mara kwa mara kwa bei ya kahawa duniani na kuathiri mipango ya wakulima nchini. Babu alisema wakulima wengi wa kahawa na wananchi hawanywi kahawa na hivyo kutegemea soko la nje hata bei inaposhuka.





# Makandarasi wanaogawa zabuni waonywa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MAKANDARASI mkoani hapa wameonywa kuacha tabia ya kugawa zabuni za ujenzi wa barabara kwa watu wasio na uwezo na kusababisha kujengwa chini ya kiwango.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba 33 ya ukarabati wa miundombinu ya barabara baina ya makandarasi na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani hapa yenye thamani ya Sh. bilioni 10.2.

Macha, alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa na tabia ya kugawa kazi na kuwalipa fedha kidogo watu ambao hawana uwezo na kusababisha ujenzi wa barabara kushindwa kukamilika kwa wakati, kutekelezwa chini ya kiwango na kuisababisha serikali hasara.

"Msiende kugawa kazi hizi kwa watu wengine, nendeni mkazifanye wenyewe kama milivyoomba kupitia makampuni yenu, tunataka barabara na madaraja yatengenezwe kwa ubora unaotakiwa na mimi nitakuwa nafanya ziara za kushtukiza ya kuzikagua," alisema.

Alisema barabara ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu katika shughuli mbalimbali ikiwamo kukuza uchumi, na kuwasihi wakandarasi hao kufanya kazi kwa bidii, weledi, uzalendo na kukamilisha ujenzi kwa wakati na ubora unaotakiwa.

**Alisema na barabara ambazo zitafanyiwa matengenezo zina urefu wa kilomita 716.64, ujenzi wa makalvati 381, madaraja manne, mitaro yenye urefu wa kilomita 5.28 na ujenzi wa barabara ...**

Meneja wa TARURA Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Avith Theodory, alisema wakandarasi walioshinda zabuni hizo ni 21, na mikataba ambayo inasainiwa ni 33 yenye thamani ya Sh. bilioni 10.2.

Theodory, alisema ukarabati huo unatumia fedha za mfuko wa barabara, tozo za mafuta na mfuko wa jimbo.

Alisema na barabara ambazo zitafanyiwa matengenezo zina urefu wa kilomita 716.64, ujenzi wa makalvati 381, madaraja manne, mitaro yenye urefu wa kilomita 5.28 na ujenzi wa barabara kiwango cha lami kilomita 2.8 na uwekaji wa taa za barabarani.

"Makandarasi waliopatikana ni kutoka mikoa mbalimbali wakiwamo wenyeji wa mkoa huu wa Shinyanga baada ya kutangaza kazi hizi kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi (NesT) mwanzoni mwa mwezi wa saba (julai)," alisema Theodory.

Mmoja wa makandarasi hao kutoka Kampuni ya Gapro Construction Limited, Mhandisi Amedeus Mselle, aliishukuru serikali kwa kuwaamini makandarasi wazawa, kuwapatia kazi na kuahidi watafanya kwa weledi na kukamilika kwa wakati.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi (kushoto), akizungumza na wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wa Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga jana, akiwa katika ziara yake maalumu ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta ya elimu na afya. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mamia wapata majisafi, salama

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

ZAIDI ya wakazi 30,000 wa Kijiji cha Chifufu wilayani hapa Mkoa wa Mwanza wameondokana na adha ya kutumia maji yasiyo salama kwa afya zao baada ya kukamilika mradi uliotekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Akizindua mradi huo katika kijiji hicho, Kiongozi wa Mbio za Mwenge Taifa, Godfrey Mnzava, alimwagiza Meneja wa RUWASA wilayani hapa kusambaza maji katika vijiji na vitongoji ambavyo bado havijafikiwa na huduma hiyo ambavyo vipo ndani ya mradi huo.

Mnzava, alivitaja baadhi ya vijiji hivyo vilivyoko Kata ya Chifufu ni pamoja na Lubanga, Nyarungombe na Lukola.

Awali akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Sengerema, Mhadisi George Massawe, alisema kukamilika kwake kutasaidia kuwatua ndoo kichwani wanawake na kuwaondolea adha kutumia muda mwingi kutafuta maji.

Massawe, alisema mradi huo utachochea utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukuaji wa mji na kuinua uchumi wa jamii kila mwanakijiji.

Alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh.bilioni 2.93, fedha zilizotolewa na serikali.

Mwenge huo katika Halmashauri ya Wilaya hiyo pia umeweka jiwe la msingi katika Kituo cha Afya Nyamazugo, kukagua jengo la kutolea huduma za dharura, uzinduzi wa ujenzi wa shule ya awali na msingi ya Isamilo, kutoa msaada wa mablanketi 100 na viti viwili vya magurudumu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

# Wataja chanzo ukatili kwa watoto

**Na Elizabeth Faustine,**
MWANZA

BAADHI ya wazazi mkoani hapa wamedai ugumu wa maisha ni chanzo cha ongezeko la vitendo vya ukatili kwa watoto kutokana na kukosa muda wa kufuatilia mienendo yao.

Wazazi hao, akiwemo Rose Shija, Mkazi wa Magu walitoa madai wakati wakizungumza na Nipashe.

Rose, alidai wazazi na walezi wanatumia muda mwingi kutafuta kipato cha kujikimu na maisha badala ya kufuatilia mienendo ya watoto wao.

Alisema yeye ni mfanyabiashara wa mboga na matunda ni mama wa watoto watano na kuwa anapata ugumu kutenga muda wa kazi na malezi ya watoto.

"Ninaamka saa 11 alfajiri kila siku kwenda sokoni kuhemea vitu vya kuuza kibandani, ninatoka kule saa nne asubuhi nikifika hapa ninapanga vitu kwa ajili ya kuuza, kule nyumbani ninamwacha binti wa kazi kwa ajili ya shughuli za nyumbani na kuangalia watoto, chakula ninakula huku huku na kurudi kwangu nyumbani ni saa nne usiku," alisema.

Alisema ratiba yake ya kazi iko hivyo kwa siku zote za wiki na kuwa kupumzika kwake ni wakati anaugua au kwenda msibani.

Alisema muda wa kukaa na watoto nyumbani anakosa japo kuna wakati anatamani kufanya hivyo.

Mwendesha bodaboda, Joseph Kenedy, Mkazi wa Igumo, alisema kazi yake inamfanya akose muda wa kukaa na familia.

Kenedy, alisema kila siku anaamka mapema watoto wakiwa bado wamelala na kurudi usiku wameshalala, hivyo kuonana nao ni kwa nadra.

Akizungumza na Nipashe Mlezi wa Watoto Kanisa Katoliki Parokia teule ya Ihayabuyaga, Paulina Pius, alisema kuna madhara mengi watoto wanayokumbana nayo kutokana na mfumo huo wa maisha.

Paulina, alisema siyo vyema kumwamini mtu kwa asilimia zote kwa ulimwengu huu kwa malezi ya watoto kwani umebadilika na ukatili dhidi yao unafanywa zaidi na ndugu wa karibu.

"Kuacha jukumu la malezi kwa binti wa kazi siyo vibaya, lakini unahitajika uangalizi wa karibu hata kama tunabanwa na majukumu, hakikisha unatenga muda wa kukagua na kufuatilia nyendo zao za siri," alisema.

Alisema wazazi wanatakiwa kutenga muda wa kuzungumza na watoto wao ili kufahamu watu wanaokutana nao, mambo wanayofanya na namna wanavyoishi na wafanyakazi wa kazi za nyumbani.




Ukurasa 12

**HASSAN NASRULLAH:**
**Kiongozi aliyeongoza mapambano kutetea wanyonge hadi shujaa muhimu vitani**



Ukurasa 13

Hata sasa Afrika inawahitaji viongozi aina ya Mwalimu



Ukurasa 14

**Ni Baba wa Taifa, kiongozi mwenye sifa kuwa mtakatifu**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 9, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


## KUELEKEA KUMBUKIZI YA NYERERE

# Ahadi 10 za mwana TANU ni muhimu zaidi sasa

• Zinafaa ziingie ndani ya katiba mpya

**Na Sabato Kasika**

JUMATATU ijayo Oktoba 14, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, anatimiza miaka 25 tangu kufariki dunia, licha ya kutwaliwa, ameacha hazina ya tunu ambazo haziwezi kuchakaa au kumaliza muda wa matumizi.

Ndiye aliyeasisi ahadi 10 za mwanachama baada ya uhuru ili kusimamia maadili na utumishi wa umma.

TANU inajiwekea ahadi hizo zilizopewa jina la 'Ahadi za Mwanachama', ili zisimamie kikamilifu kwa ajili ya kuimarisha chama na ustawi wa taifa kwa ujumla.

Tukijikumbusha ahadi ya kwanza anasema, binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja, ya pili ni utumishi; nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote, huku ya tatu ikiahidi kujitolea nafsi na nguvu kuondoa umaskini, ujinga, magonjwa na dhuluma".

Vilevile kuna ahadi ya nne inakataa ufisadi; "rushwa ni adui wa haki. Sitapokea wala kutoa rushwa. Ya tano ni 'cheo ni dhamana, sitakitumia cheo changu wala cha mwingine kwa faida yangu".

Lakini ipo ya kutafuta elimu ni ahadi ya sita, ikisema; "nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote, ya saba inasema;

Nitashirikiana na wenzangu wote kuijenga nchi yetu".

Ya nane inasema; "nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko, wakati ahadi ya tisa inakumbusha kuwa 'nitakuwa mwanachama mwaminifu wa TANU na raia mwema wa Tanganyika na Afrika".

Pamoja na hizo, ahadi ya mwisho ambayo ni ya 10, inasema; "nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa Rais wa Serikali ya Tanganyika".



Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

Nchi inapokaribia kilele cha kumbukumbu ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, Nipashe inazungumza na baadhi ya wadau wa siasa ili kupata maoni yao kuhusu ahadi hizo na kama zina nafasi bado na iwapo zinahitaji kuendelezwa.

### ZIWE KWENYE KATIBA

Ni msimamo wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, anasema ili ahadi hizo zifanye kazi, ni vyema mchakato wa katiba ufanyike na kuziingiza huko ili zisimamiwe vizuri.

"Ahadi nyingi kati ya hizo 10, hazigusi siasa, hivyo ni vyema zikaondolewa kwenye chama na kuingizwa kwenye katiba mpya ili zipewe uzito mkubwa na unaostahili," anasema Dk. Anna.

Anafafanua kuwa licha ya kuwapo kwa ahadi hizo, ambazo zinatakiwa kusimamiwa na wanachama wenyewe, bado mambo yanakwenda kinyume na jinsi yanavyotakiwa kutekelezwa.

"Kwa mfano ripoti nyingi za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinaonyesha kuwapo kwa rushwa na ufisadi katika taasisi mbalimbali pamoja na za umma, kitendo kinachoonyesha kuwa ahadi ya nne haizingatiwi," anasema.

Anasema kile ambacho Mwalimu Nyerere alikuwa akikipigania kupitia ahadi hizo inaelekea kimekwama kutokana na kuwapo vitendo ambavyo vinavyofanywa na baadhi ya wanachama kinyume na inavyotakiwa.

"Vilevile, kuna ahadi ya umoja, nitashirikiana na wenzangu wote kuijenga nchi yetu, cha ajabu tunashuhudia jinsi ambavyo wanasiasa wanabaguana hadharani, wakisema sehemu ambayo wapigakura wamechangua upinzani, serikali haiwezi kuleta maendeleo, inakuwaje," anahoji?

Anaeleza kuwa, kauli ya aina hiyo ni kinyume na ahadi za mwanachama hasa ya saba inayohimiza ushirikiano kwa ajili ya ujenzi wa taifa, na kuongeza kuwa sehemu ya ahadi hizo haifanyiwi kazi.

"Kwa maoni yangu, CCM iachiwe sehemu ya ahadi ya tisa inayosema; nitakuwa mwanachama mwaminifu wa TANU/CCM lakini upande wa kuwa raia mwema wa Tanzania na Afrika uingizwe katika katiba," anasema.

### ZIMEONDOKA NA MWALIMU

Kada wa CHADEMA, Suzan Lyimo, anasema, ahadi hizo zilitekelezwa enzi za Nyerere lakini ameondoka nazo baada ya kufariki dunia.

Anafafanua kuwa hazitelekezwi kama ilivyokusudiwa na zimepuuzwa.

Anatoa mfano ahadi ya nane; "nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko", kwamba siku hizi anayesema ukweli hatakiwi, anaonekana ni adui ndani na hata nje ya chama.

"Ukweli ni kwamba Nyerere ameondoka na ahadi za mwanachama, kwani kuna mengi yanaendelea kufanywa kinyume na malengo ya ahadi hizo 10 kana kwamba hazipo," anaeleza Suzan.

**INAENDELEA UK. 13**

## HASSAN NASRULLAH:

# Kiongozi aliyeongoza mapambano kutetea wanyonge hadi shujaa muhimu vitani

**Na Mwandishi Wetu**

SAYYID (baba) Hassan Nasrullah, aliyejulikana kama Sayyid wa viongozi wa ulimwengu wa Kiarabu, alipewa jina la Sayyid wa muqawama (mapambano) na ukombozi.

Ni kwa sababu ya msisitizo wake hasa kwenye kanuni na maadili katika kuwatetea wanaodhulumiwa, pamoja na mapambano yake makali dhidi ya ubeberu.

Mtaalamu wa Ushauri wa Kitamaduni wa Ubalozi wa Iran nchini Tanzania Maulid Sengi, anamzungumzia shahidi Nasrullah, akisema alizaliwa Agosti 31, 1960 katika Kijiji cha Al Bazourieh Kusini mwa Lebanon.

Mwaka 1976 akiwa kijana, alikwenda Najaf, Iraq, kuanza masomo katika seminari na kurejea Lebanon 1978, akiendelea na masomo katika Shule ya Imam al-Muntazar (a.s.).

Ilianzishwa na Sayyid Abbas Mousawi, Katibu Mkuu wa zamani wa Hizbullah, na wakati huo huo, alijishughulisha na siasa katika eneo la Bekaa.

Baada ya kuasisiwa Hizbullah, Nasrullah alishika nyadhifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na uanachama katika Baraza la Uongozi la Hizbullah, lakini hakujiweka mbali, akiendelea kutafuta elimu hadi alipokwenda Qum nchini Iran, 1989 kukamilisha masomo yake.


Sengi anasema mashambulizi makubwa ya Israel dhidi ya Lebanon na mapambano ya Hizbullah dhidi ya utawala huo hayakumruhusu kukaa Qum kwa zaidi ya mwaka mmoja, alirejea Lebanon kwa mara nyingine na kujiunga na wenzake katika kukabiliana nayo.

Mwaka 1992, Abbas Mousavi, Katibu Mkuu wa Hizbullah wakati huo na mwalimu wa Nasrullah aliuawa.

"Kupanda ngazi kwa Nasrullah katika harakati hiyo, kuliiondoa Hizbullah katika mzingo wa ulinzi na usalama na kufungua medani mpya ya uwepo wa Hizbullah katika muundo wa kisiasa wa Lebanon.

"Mwaka wa 2000, wakati wa mazungumzo kati ya Yasser Arafat na maofisa wa Marekani na Israel ili kutatua mzozo katika eneo la Asia Magharibi yaliyokwama. Jeshi la Israel lilijiondoa katika maeneo yaliyokuwa yakikaliwa kwa mabavu ya kusini mwa Lebanon katika hatua ya upande mmoja na bila ya kupata lolote kutoka Hizbullah.

"Majeshi la Israel yaliondoka katika maeneo yote yaliyokaliwa kwa mabavu, isipokuwa mpakani na mashamba ya Shabaa."



Sayyed Hassan Nasrallah, enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

> Mwaka wa 2000, wakati wa mazungumzo kati ya Yasser Arafat na maofisa wa Marekani na Israel ili kutatua mzozo katika eneo la Asia Magharibi yaliyokwama.

Sengi anasema kushindwa huko mbali na kuimarisha msimamo wa Hizbullah kama harakati ya mapambano, kulimfanya Nasrullah apate mafanikio makubwa kati ya Waarabu na Waislamu kwa ujumla.

"Kuanzia hapo akatambuliwa kama mtu muhimu zaidi katika ulimwengu wa Kiarabu," anasema Sengi.

Anasema kwa upande mwingine, kwa kuegemea kwenye mafanikio hayo, Hizbullah ya Lebanon iliimarisha uwepo wake katika uga wa kisiasa kwa kadiri kwamba, mbali na kushinda viti vingi vya bunge, pia ilishika usukani wa idadi ya wizara za serikali ya nchi hiyo.

Juhudi zisizokoma za Hassan Nasrullah katika kutetea haki za wanyonge na kubeba bendera ya Kambi ya muqawama kwa miaka mingi, ziliandamana na mafanikio na ushindi wa wapiganaji .

Jambo hilo lililomfanya Nasrullah daima kuwa miongoni mwa walengwa wakuu wa idara za ujasusi na utawala wa Israel.

Anasema baada ya miaka mingi ya misimamo ya kishujaa na juhudi kubwa za kuendeleza kambi ya mapambano na muqawama, jioni ya Ijumaa Septemba 27, 2024 Hassan Nasrullah, aliuawa.

"Alifanikiwa kupata daraja ya juu ya kuuliwa shahidi katika jinai ya utawala wa Israel na mashambulizi yake dhidi ya makazi ya raia eneo la Dhahiya, kusini mwa Beirut."

Nasrullah alikuwa ni Katibu Mkuu wa tatu wa Hizbullah, chama cha kisiasa na kijeshi cha Lebanon kilichoasisiwa mwaka 1982.

Chini ya uongozi wake, Hizbullah iliimarika na kuwa na nguvu muhimu ya kikanda iliyofanikiwa kuilazimisha Israel kuondoka Kusini mwa Lebanon mwaka 2000, baada ya operesheni za kijeshi zilizojumuisha kuwarudisha huru wafungwa wa Kilebanoni.

Hassan Nasrullah aliuawa kwa mashambulizi ya anga yaliyofanywa na vikosi vya Israel

na kuongezeka kwa tofauti kati ya Hizbullah na harakati za kikundi cha Amal, hali iliyosababisha Baraza la Uongozi kumtaka arudi nyumbani.

Mwaka 1978, Hassan Nasrullah akiwa na umri wa miaka 18, alifunga ndoa na Fatimah Yassin. Akijaliwa kupata watoto watatu wa kiume ambao ni Muhammad Hadi, Muhammad Jawad na Muhammad Ali, pamoja na binti anayeitwa Zaynab.

Muhammad Hadi, mtoto mkubwa, aliuawa Septemba 12, 1997 Miladia, katika mapambano dhidi ya vikosi vya ulinzi vya Israel Kusini mwa Lebanon.

Mwili wake ulibakia mikononi mwa Israel na baada ya mwaka mmoja, ulirejeshwa Lebanon kupitia operesheni ya kubadilishana wafungwa kati ya Israel na Hizbullah.

Shughuli za kijamii na kisiasa za Hassan Nasrallah zilianza tangu akiwa mdogo.

Baada ya kumaliza sekondari mwaka 1975 Miladia, aliteuliwa kuwa kiongozi wa kikundi cha harakati za Amal katika kijiji chake cha al-Bazuriyya.

Baada ya kurejea kutoka Najaf mwaka 1979, alijiunga na ofisi ya kisiasa ya harakati za Amal na kuwa mwakilishi wa harakati hizo katika bonde la Biqaa.

Mwaka 1982, akiwa pamoja na kundi la wanazuoni na wanafunzi wa kidini waliohamasishwa na mapambano, alijitenga na kundi la harakati za Amal na kuanzisha kundi la Hizbullah ya Lebanon.

Kuanzia mwaka 1982 hadi 1992 Nasrullah alitumia muda wake wote Hizbullah na kwamba mbali na kuwa mjumbe wa Baraza Kuu la Hizbullah, pia alishiriki kuandaa vikosi vya upinzani na kuanzisha vikundi mbalimbali vya kijeshi.

Alikuwa Naibu wa Ibrahim Amin al-Sayyid, kiongozi wa Hizbullah mjini Beirut, na kwa kipindi fulani alikuwa ni Naibu Mtendaji wa Hizbullah ya Lebanon.

Sengi anasema Hassan Nasrallah alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Hizbullah ya Lebanon kwa makubaliano ya wanachama baada ya kuuawa kwa Abbas Mousawi, Februari 16, 1992, akichukua jukumu hilo akiwa na miaka 32.

Kwa kuangalia mchango wake binafsi pamoja na jitihada za Hizbullah kukomboa Kusini mwa Lebanon mwaka 2000, baada ya miaka 22 ya uvamizi wa Israel, pamoja na ushindi katika vita vya siku 33, Hassan Nasrullah, alipatiwa jina la "Sayyid wa upinzani au baba wa upinzani".

# Hata sasa Afrika inawahitaji viongozi aina ya Mwalimu

**Na Gaudensia Mngumi**



Mwalimu Nyerere (wa pili kushoto) akiwa na baadhi ya marais Milton Obote wa Uganda (kushoto), Jomo Kenyatta wa Kenya (wa pili kulia ) na Kenneth Kaunda wa Zambia. **PICHA: MTANDAO**

MIAKA 25 baada ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, tunapoitazama Afrika kuna mengi ya kujifunza hasa kuhusu uongozi bora ili kuibadilisha iwe bara tajiri badala ya fukara.

Nyerere anabaki kuwa kiongozi ambaye hakuwa na tamaa binafsi wakati wote wa uhai wake, akikumbukwa kuwa alikuwa na chuki kali dhidi ya utajiri na kusaka pia mali na kujilimbikizia utajiri haramu.

Hakuthamini pesa au vitu kama nyumba, mashamba, fedha za kigeni na chochote kilichokuwa ni cha kimwili. Aliwathamini watu, taifa na maendeleo ya wote.

Kuna wakati alisema pesa si ni matokeo, akimaanisha kwamba cha muhimu na juhudi na kujituma si kufikiria pesa.

Miongo miwili baada ya kifo chake Afrika, aliyoipenda bado ni maskini. Lakini hili ni bara maskini kweli? Ni imani ambayo watu wanayo na viongozi wanaikubali na kuendelea kuishikilia.

Ni rahisi kwa yeyote kuona utajiri wa bara hili iwe kwenye machapisho kuanzia magazeti, runinga, vitabu, 'dokumentari' lakini hata ukitembea kwenye mataifa mbalimbali unaushuhudia.

Mfano, yapo mabonde na nyanda za kilimo, maji ya bahari, mito na maziwa, misitu yenye miti na uoto unaofaa kufuga nyuki na kuzalisha asali na mbuga na hifadhi za wanyama pori.

Yote hayo yamesikika na kuonekana kila mwaka, watu wanaposoma kuhusu Afrika wanathibitisha namna ilivyo nchi nzuri lakini mbona ni maskini?

Afrika Kusini ya Sahara Tanzania ikiwa sehemu ya hayo, nchi zenye madeni makubwa duniani zikidaiwa Dola za Marekani trilioni 1.15.

Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADF), inafafanua zaidi kwamba deni lake la nje lilikuwa Dola trilioni 1.12 mwaka 2022 lakini kufikia mwisho mwa 2023 liliongezeka na kufikia trilioni 1.152.

Licha ya kuwapo deni hilo kubwa la nje, lipo la ndani pia. Cha kushangaza nchi hizo zina pesa nyingi zinazopokea kama mikopo, misaada, fedha nyingine kutoka kwa 'dayaspora' wanaotuma pesa na misaada nyumbani na rasilimali za kila aina. Swali, mbona hatutoki na ufukara unaongezeka?

Mwalimu Julius Nyerere mwanamajumuiya wa Afrika pamoja na kushiriki kikamilifu katika kukomboa Afrika na kuanzisha Umoja wa Afrika wa Nchi Huru za Afrika (OAU) aliona ulazima wa viongozi kujilikana wenyewe na kuacha kuutumikia mwili ili kuisaidia Afrika.

Ni kiongozi aliyeamini kwamba kuwa na tamaa za ubinafsi kusingeisaidia Afrika kufikia maendeleo. Aliona kuwa ni lazima kuwa mtumishi mwaminifu wa watu na kusimamia kuwapo na ushirikiano kuanzia kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa sababu isingekuwa rahisi kwa Afrika kuendelea, maana dunia na ubeberu husingeweza kuliruhusu hilo.

Maono ya Nyerere yalikuwa ni kufikia ukombozi wa kweli na kutetea umoja wa Afrika kiuchumi, kisiasa na zaidi kujiletea maendeleo kwa nguvu zao wenyewe.

Viongozi wenye maono kama ya Nyerere wanahitajika zaidi Afrika kwa sasa kuliko wakati mwingine, ni ili kuifanya Afrika ijitegemee, iendelee kiuchumi na kisiasa kwa kutumia rasilimali, watu wake na zaidi juhudi zake.

Umaskini unaelezwa kuwa unaendelea kuongezeka kwa sababu ya rushwa, wizi na ubadhirifu wa fedha za umma. Wakati mwingine ukwepaji mkubwa wa kodi.

Upo wizi kupitia mikataba tata inayoandaliwa na watendaji na wanasheria wa Afrika, watu kuiba fedha kupitia ujenzi duni wa miradi ya umma, kuanzia barabara na majengo, kilimo, madini na kzi kwa ujumla hufanywa chini ya kiwango.

Kuna gharama kubwa za kuendesha serikali kubwa, zenye vitendeakazi vya kifahari, mishahara na posho nono na zaidi sana kujitajirisha.

Suala la rushwa na kujilimbikizia mali Mwalimu Nyerere, alilipiga sana vita. Akiandaa miongozo ya viongozi na pia kuwahimiza Watanzania viongozi kuziishi ahadi za TANU.

Ahadi za Mwana TANU za kupinga rushwa na kuwa mzalendo kutumikia nchi kwa moyo wote zinahitajika zaidi wakati huu kukabili wabadhirifu na wahujumu uchumi hasa wala rushwa.

Kwa mfano Jumapili iliyopita, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anaagiza kushtakiwa mara moja maofisa wanne wa Manispaa ya Kigamboni Dar es Salaam na watumishi wanne wa kitengo cha akaunti jumuifu ya amana (TSA) TAMISEMI kwa tuhuma za ubadhirifu wa Shilingi milioni 165.6.

Anaagiza mtumishi wa kitengo cha akaunti jumuifu ya amana asimamishwe kazi kwa tuhuma za kushiriki kwenye muamala uliohamisha fedha kutoka TAMISEMI kwenda Manispaa ya Kigamboni.

Kwa kuangalia halmashauri moja ya Kigamboni milioni 100 inachotwa na watu wachache, vipi kitaifa kuna mitandao mingapi ya aina hiyo inayohujumu uchumi na fedha za umma?

Si tatizo la Tanzania pekee ni la Afrika nzima na yapo baadhi ya mataifa ambayo viongozi wakuu au wana familia zao ndiyo mabilionea maarufu duniani, wakijilimbikizia mali na utajiri wa nchi zao mifukoni.

Tena viongozi wanasifika kusaidia makampuni ya kimataifa kukwepa kodi, ruksa za kuhujumu uchumi kupitia 'vimemo' zikitolewa na ikulu.

Pamoja na viongozi wakuu wa mataifa kuhujumu nchi, tatizo la mawaziri na watendaji wakuu wa serikali ndiyo wanaotuhumiwa kuficha fedha za umma kwenye akaunti nje ya mataifa yao.

Ikumbukwe Nyerere aliishi maisha ya kawaida sana. Hakuwa na makuu, alivaa kawaida, nguo rahisi ambazo zilikuwa si za gharama. Alifahamu kuwa Tanzania ni nchi yenye joto si taifa la suti na tai.

Leo Tanzania na Afrika zinapomkumbuka Nyerere viongozi wana nafasi ya kumuiga, kwanza kuachana na tamaa za kumiliki mali nyingi kwa kuibia hazina za mataifa yao.

Tena kuachana na kuweka tamaa za utajiri za kumiliki ndege, magari ya kifahari, kutembea na misafara ya magari lukuki, kuepuka mapambo hasa saa za dhahabu, viti ghali zaidi na almasi pamoja na mavazi ya kila mitindo tena kwa gharama za raia wake, huku wananchi wakiishi bila mlo wa siku.

## Ahadi 10 za mwana TANU ni muhimu zaidi sasa

**INATOKA UK. 11**

Mbunge huyo wa zamani wa CHADEMA, anataja rushwa, akisema zamani ni adui namba moja wa haki na maendeleo. Kwa sasa imekuwa si adui wa haki wala mkwamishaji maendeleo pengine ni rafiki wa watu. Kwa kuwa wengi wanatoa na kupokea kama jambo la kawaida badala ya kuikimbia.

Imepewa majina mengi ikiwamo takrima.

"Tuambiane ukweli bila kificho kuwa, ahadi 10 za mwanachama ni kama hazipo tena, kwani tukianza kutaja mambo yanayotendeka kinyume na ahadi hizo ndani ya nchi ni mengi," anasema.

Anasema ahadi hizo zinapinga ubaguzi, wa rangi, kabila, dini na aina myingine za kubaguana na kuhimiza umoja na mshikamano, lakini badala yake Watanzania sasa wanabaguana kwa itikadi za vyama vya siasa.

Mwaka huu kuna mwanachama wa CCM alitamka hadharani kuwa wanapowapoteza watu, polisi wasihangaike kuwatafuta watu hao, kitendo kinachokwenda kinyume na ahadi zao wenyewe, anasema.

Anasema ahadi zote 10 zilikuwa na lengo zuri, na kwamba zimekwama kufichwa kazi kwa kukosa usimamizi na kusababisha wachache wanaojaribu kuzisimamia, kuonekana kama maadui.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ni Baba wa Taifa, kiongozi mwenye sifa kuwa mtakatifu

**Na Dk. Peter Kafumu**

JULIUS Nyerere, anayefahamika kama 'Mwalimu' alizaliwa Aprili 13, 1922 katika Kijiji cha Butiama mkoani Mara na akafariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, Uingereza.

Alikuwa kiongozi maarufu aliyeshiriki kwa juhudi kubwa kuleta umoja wa Afrika, akiwa mpigania umoja hodari aliyeamini kuwa maendeleo yatafanikiwa tu kama mataifa ya Afrika yataungana kuwa taifa moja.

Alishiriki kuanzisha Muungano wa Umoja wa Afrika 'Organization of African Unity (OAU)' 1963. Umoja huu ulipanga kukuza mshikamano wa kufanya kazi kwa pamoja.

Amesaidia kwa nguvu zote kwenye ukombozi wa Afrika. Katika juhudi hizo vyama vya ukombozi vilianzisha makao yake makuu Tanzania mfano MPLA cha Angola; SWAPO cha Namibia; ANC na PAC vyote vya Afrika Kusini, FRELIMO cha Msumbiji na ZANU cha Zimbabwe. Kujitolea na kujitoa kuleta ukombozi na kutetea umoja wa Afrika kumeacha urithi wa kumbukumbu ya kudumu kwa Mwalimu.


Kwa Watanzania, Mwalimu Nyerere alionyesha huruma na upendo kwa watu wake pamoja na kuwa tulikuwa taifa lenye makabila zaidi ya 120 alitufundisha kupendana na kuwa wamoja kama nchi moja. Umoja wa Watanzania ulimarishwa zaidi na maono ya Mwalimu aliyotoa Oktoba 22, 1959 kwenye hotuba yake aliyoitoa bungeni wakati huo likijulikana kama Legico aliposema "... Sisi watu wa Tanganyika tunataka kuuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro umulike hata nje ya mipaka yetu, ulete tumaini pale ambapo hapana matumaini, upendo pale ambapo pana chuki na heshima palipojaa dharau..".

Siku ya Uhuru wa Tanganyika, maono yake yalitimia pale Kapteni Nyirenda wa Jeshi la Tanganyika aliposimika Mwenge kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro umulike nje ya mipaka.

Na tangu siku hiyo Mwenge wa Uhuru ulianza kikimbizwa nchi nzima kila mwaka ukiwasha kila mahali roho ya moto wa uhuru, umoja, amani, na upendo miongoni mwa Watanzania.

Umoja wetu Watanzania uliimarishwa zaidi kwa kutumia Kiswahili kama lugha ya taifa ambayo Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliihamasisha kwa juhudi kubwa.

Alipinga kwa nguvu zote aina zote za ubaguzi uwe wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, rangi, kikabila, na kidini. Alikuwa kiongozi shupavu aliyeikataa rushwa. Hakujilimbikizia mali, hali ambayo alipostaafu serikali ilibidi imjengee nyumba ndogo pale kijijini kwake Butiama, ambayo hata leo ipo.



Mwalimu Julius Nyerere akiwasha Mwenge kuwapa raia matumaini ya moto wa uhuru usiozimika ndani ya taifa. **PICHA: MTANDAO**

> Alishiriki kuanzisha Muungano wa Umoja wa Afrika 'Organization of African Unity (OAU)' 1963. Umoja huu ulipanga kukuza mshikamano wa kufanya kazi kwa pamoja.

Alikuwa mkali sana kwa viongozi na watumishi wa serikali walioonekana kujilimbikizia mali wakati wa utumishi wao serikalini. Ili kupambana na hali hiyo mwaka 1971 aliandika Mwongozo wa TANU uliotoa makatazo kwa viongozi na watumishi wa umma kutoa na ama kupokea rushwa ili kuwa na mali nyingi badala ya kufanya kazi za kuwahudumia wananchi kwa heshima.

Uadilifu, unyenyekevu, ucha Mungu na akili nyingi za Mwalimu Nyerere vilikuwa ni dira ya namna alivyoliongoza taifa na tabia yake hiyo imelihamasisha Kanisa Katoliki kuamini kuwa alikuwa kiongozi mkuu mwenye hulka za kimalaika na mwaka 2005, Maaskafu wa Kanisa Katoliki wa Tanzania kwa kibali kutoka Vatikan Makao Makuu ya Kanisa walianzisha mchakato wa kutangazwa Mwenye Heri na baadaye kuwa Mtakatifu.

Viongozi wa Kanisa pamoja na baadhi ya wasomi wameendelea kuamini kuwa Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mwadilifu na mwema wa kuigwa na viongozi wengine wa nyakati zetu hizi.

Leo Afrika inakabiliwa na ombwe kubwa la uongozi kwa sababu wengi wanajihusisha na rushwa wakijilimbikizia mali kwa ajili ya maisha binafsi. Ukiwalinganisha na Mwalimu Nyerere ambaye anaelezwa na Papa Francis kwenye Waraka wake wa Kichungaji wa Evangelii Gaudium 273 kuwa ni kiongozi "Mwanasiasa Mwenye Nafsi" aliyeishi kwa kujitoa kwa ajili ya wengine, tofauti na viongozi wengine walioshi na wanaoishi kwa ajili ya manufaa yao wenyewe na hivyo ni viongozi walioleta na wanaoleta fedheha Afrika.

Daktari Ng'wanza Kamata wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anaandika kuhusu Mwalimu Nyerere akionyesha utangamano wa maisha yake kisiasa na kidini. Akisema: "...Mwalimu Julius Nyerere, alipigania maendeleo ya watu, alitafuta kuwawezesha maskini wa taifa lake, na akasimamia uwepo wa heshima na haki za binadamu na uvumilivu wa kidini katika taifa lenye dini nyingi. Akiwa Mkatoliki imara kila mara alisoma na kutafakari Maandiko Matakatifu na alitafsiri kwa Kiswahili baadhi ya miongozo ya ibada akitoa ushauri juu ya kulifanya kanisa kuendana na jamii ya nyakati zilizopo. Aliishi maisha ya kawaida..." Masimulizi ya Dk. Kamata yanaonyesha kuwa maisha ya kisiasa na ya kidini ya Mwalimu Nyerere hayakukinzana na ndiyo yaliyomfanya Mwalimu kuwa kiongozi mzuri na mkweli.

Kwenye Mkutano wa Kimataifa ulioitwa "the International Colloquium on "Mwalimu Julius Nyerere a Politician with a Soul and a Servant of God" uliofanyika Novemba 21, 2023 Mjini Roma kuangalia uhusiano wa imani na siasa katika maisha ya Mwalimu Nyerere; Askofu Mkuu Fortunatus Nwachuku wa Idara ya Mafundisho kuhusu Imani, Vatican akitoa mada katika mkutano huo anasema:

"...Mwalimu Nyerere akiwa Rais kipaumbele chake hakikuwa kuwa na fedha nyingi katika akaunti yake ya benki mahali fulani huko Ulaya, kipaumbele chake kilikuwa ni kuwaunganisha watu...msisitizo wake haukuwa kwenye wingi wa magari anayomiliki; kipaumbele chake kilikuwa juu ya ujamaa, yaani namna ya kuwaunganisha watu ili wawe pamoja kama kaka na dada..."

Mchakato wa kumtangaza Nyerere kuwa Mtakatifu ni ushahidi tosha kwamba alikuwa kiongozi mwenye huruma na upendo aliyeishi kama ukweli. Kanisa Katoliki linasali pamoja na dunia nzima husala sala hii ili Mungu audhihirishe Utakatifu wa Julius Kambarage Nyerere katika maisha yake baada ya kifo. Na hapa tunasali:

Ee Mungu Baba Yetu, ulitumba na kutuweka duniani ili tukujue, tukutumikie, tukupende wewe na tuwapenda ndugu zetu.

Baba Muumbaji, tunakushukuru kwa ajili ya zawadi ya mtumishi wako Julius Kambarage Nyerere - mwamini mlei na baba wa familia aliyewaongoza watu wako wa taifa la Tanzania kama Baba na Mwalimu kweli.

Ee Baba mtumishi wako alijitoa kabisa kwa ajili ya watu wako kwa mapendo yasiyo na mipaka akijenga bila kuchoka umoja na mshikamano wa watoto wote wa Mungu. Aliwajalia maskini, aliwainua wanyonge, aliwafariji yatima na wote waliokimbia makwao kwa kukosa amani aliwakaribisha kwa furaha na kuwatunza. Ee Mungu, Mtumishi wako alikuwa mwaminifu kwako na kwa kanisa lako, akawa kweli kielelezo cha imani hai na uchaji halisi. Alijawa upendo mkubwa na heshima kwa Mama mzazi wa Mwanao na Bwana wetu Yesu Kristu, akawakabidhi raia wa nchi yake kwa Bikira Maria wawe salama chini ya ulinzi wake wa kimama.

Ee Mungu Mtumishi wako Julius Kabarage Nyerere alionyesha ari kubwa ya kuwafundisha watu wote kukutambua na kukuheshimu, alitetea haki na kupinga uonevu na unyanyasaji wa aina zote. Huduma yake nyenyekevu kwa watu wa Mungu imebaki mfano wa kuigwa kwa watu wa vizazi vyote katika safari yao ya kuelekea kwako.

Mungu Baba Mwenyezi, tunakusihi sana utujalie fadhila tunazokuomba kwa maombezi yake, kadiri ya mapenzi yako matakatifu, kusudi utakatifu wa mtumishi wako udhihirike wazi kwa watu wote wa taifa la Mungu aweze kutangazwa mapema kuwa mmoja wa watakatifu wako. AMINA.

***Mwandishi ni mbunge wa zamani wa Igunga (CCM) na Kamishna wa Madini mstaafu.***



## HABARI DODOMA

# Serikali yajizatiti kukabili maafa nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderianaga ametaja hatua tisa zilizochukuliwa na serikali katika usimamizi wa maafa kuanzia mwaka 2020 hadi sasa.

Nderianaga alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo kwa waratibu wa maafa wa wizara, taasisi, mashirika ya umoja wa mataifa, kimataifa na asasi za kiraia.

Alisema hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Maafa namba 6 na kanuni za mwaka 2022.

Alisema shughuli za usimamizi wa maafa zinahitaji kuwa na utayari kwa kuweka mipango na mikakati miongoni mwa wadau wa sekta husika.

"Tumekuwa tukihakikisha sera, sheria, mikakati, mipango na miongozo ya usimamizi wa maafa inakuwapo, inaeleweka na kuwafikia wadau na wananchi katika kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji na hatua zilizokusudiwa," alisema Nderianaga.

kuendesha mazoezi ya nadharia ya kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa majanga ya mafuriko, vimbunga na Tsunami.

Kuimarisha maghala ya kuhifadhi vifaa vya msaada katika kanda sita nchini, kuongeza vifaa vya kutolea huduma za kibinadamu na kutoa vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa wananchi walioathirika na maafa katika halmashauri nchini.

Kufanya mafunzo kwa kamati za usimamizi wa maafa za mikoa na wilaya na voluntia, kutoa elimu kwa umma, wataalam wa asasi za kiraia kutoka redio za kijamii nchini na kuandaa mipango ya wilaya kujiandaa na kukabili na hali hiyo.

Kuanzisha chumba cha kufuatilia mwenendo wa majanga na utoaji wa tahadhari za mapema katika Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura chenye vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na pamoja na mifumo ya kufuatilia mwenendo wa majanga na kufanya tathmini ya hali ya uwezekano wa kuathirika ili kutoa tahadhari kwa wakati kwa ajili ya jamii husika kuchukua hatua.

> **Hata hivyo, alisema matukio ya maafa yanayosababishwa na majanga ya asili na shughuli za kibinadamu yamekuwa yakiongezeka na kuathiri maisha ya watu...**

Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa katika eneo la Nzuguni B jijini Dodoma, unaojumuisha maghala mawili na jengo la utawala na kuimarisha uwezo wa vifaa vya kukabiliana na maafa na uokozi.

Hata hivyo, alisema matukio ya maafa yanayosababishwa na majanga ya asili na shughuli za kibinadamu yamekuwa yakiongezeka na kuathiri maisha ya watu, mali zao na kuleta madharaya kijamii na kiuchumi.

Alisema mafunzo hayo yataimarisha utendaji kazi wao kwa kuzingatia sera na sheria na miongozo ikiwamo Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa (2022), Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wakati wa Maafa (2022), Mpango Mkakati wa Taifa wa Afya Moja (2022-2027).

Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), Patrick Codja, aliipongeza serikali kwa kuimarisha shughuli za usimamizi wa majanga.

"Uratibu wa majanga unahusisha pia utayari na uharaka wa serikali katika kuyashughulikia. Juhudi za serikali zimeshuhudiwa katika majanga mbalimbali yaliyojitokeza hapa Tanzania mwaka 2023 na la hivi karibuni la Kimbunga Hidaya," alisema.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Eleuter Kihwele, alisema mafunzo hayo yanatarajiwa kuleta mchango mkubwa kukabiliana na maafa nchini.




Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ramadhani Kingai (kulia), akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Menejimenti ya Taasisi zinazounda UTATU ambazo ni Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Jeshi la Polisi kupitia Kamisheni ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), jijini Dodoma jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

## DUWASA yaanzisha mradi kwa wenye kipato cha chini

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) imeanzisha mradi kwa ajili ya kuunganishia huduma ya majisafi na salama kwa kaya zenye kipato cha chini kwa gharama nafuu.

Mratibu wake, Mary Godfrey aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mradi huo uitwao 'Water for Life'.

Kwa mujibu wa Mary, mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Uholanzi kwa gharama ya Sh. milioni 900 na DUWASA watatoa nguvu kazi kuukamilisha.

Alisema mradi huo ambao utaanza katika kata za Nzuguni, Ntyuka na Mnadani, unatarajiwa kuwaunganishia huduma hiyo kaya 1,250.

"Kuna mitaa michache ambayo imetambuliwa katika upembuzi ulioanza mwaka 2022, vigezo kwa wanufaika ni kuwa na utayari wa kulipa gharama za maunganisho ya maji ambayo ni Sh. 30,000 tu na uwezo wa kulipa ankara za maji kila mwezi kulingana na matumizi," alisema.

Mary, alisema makundi maalum kama wazee, watu wenye ulemavu na kaya zenye kipato cha chini pamoja idadi ya wategemezi hao, watapewa kipaumbele katika mradi huo.

Mkurungenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema lengo la mradi huo ni kuongeza idadi ya wananchi kufikiwa na huduma ya maji safi na salama.

Joseph, alisema hadi sasa DUWASA ina wateja 84,310 kwa Jiji la Dodoma, Chamwino Ikulu, Kongwa na Bahi.

Aliwataka wafanyakazi wa mamlaka hiyo kuendelea kuwa na lugha nzuri wakati wa kuwahudumia wateja wao ili kupunguza malalamiko .

Alisema katika maadhimisho ya huduma kwa wateja, watawatembelea wateja wakubwa na wadogo na kuzungumza nao kuhusu utoaji wa huduma ya maji.

# Wazazi wahimizwa kuzingatia malezi ya watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewataka wazazi kuwalea watoto katika misingi ya dini, mila, desturi na tamaduni ili kuwaepusha kujiingiza katika uhalifu.

Dendego alitoa rai hiyo juzi wakati akizindua Bodi ya Parole katika Ofisi za Jeshi la Magereza mkoani hapa.

Alisema kuwa ametoa rai hiyo kutokana na takwimu kuonyesha kuna ongezeko kubwa la vijana wanaojihusisha na vitendo hivyo, wakiwamo waliomaliza vifungo vyao gerezani, hali ambayo inahitaji wazazi kusimamia malezi kwa watoto wao.

"Wazazi warudi katika majukumu yao ya msingi ya kulea watoto, tusiache nafasi kubwa kwa watoto kujifunza katika mifumo kama mitandao ya kijamii bali tuwalee katika misingi ya dini, mila, desturi na tamaduni zetu," alisema.

Dendego aliipongeza bodi hiyo kwa utendaji wa kazi huku akisisitiza elimu kutolewa kwa wananchi ili kuelewa zaidi majukumu yake na umuhimu wake kwa walengwa wa moja kwa moja ili kuendelea kunufaika na fursa hiyo.

Mwenyekiti wa bodi hiyo mkoani Singida, Liana Hassan, aliahidi kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutekeleza kazi na kusisitiza utayari katika kufanya kazi na ushirikiano baina yao kwa maslahi ya jeshi hilo na Taifa.

"Tutatoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa kazi hii ambayo tumeaminiwa kuifanya, serikali yetu imetuamini," alisema.

Katibu wa bodi hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Magereza wa Mkoa huo, Khatibu Semzono, alisema parole kama utaratibu wa sheria unaotoa fursa kwa wafungwa waliofungwa kuanzia miaka minne waliokwisha kutumikia theluthi ya kifungo chao na kuonyesha uelekeo wa kurekebika na tabia nzuri kurudi katika jamii kwa masharti maalumu na kanuni.

Alisema vigezo vinavyopendekezwa na kunufaika na Parole ni maoni ya viongozi wa vijiji au aina ya makosa, maoni ya familia, upatikanaji wa waathirika na maoni yao hasa kwa jamii ya wafugaji ambao hawana makazi maalum.

Vingine ni upatikanaji wa nyaraka za hukumu na alama za vidole kwa wakati, mienendo na tabia wawapo gerezani na taarifa kutoka kitengo cha upelelezi.



# CCM yaiagiza serikali kukamilisha mradi wa maji

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, kimeiagiza serikali kukamilisha kwa wakati mradi wa maji wa Kijiji cha Mawengi kilichoko Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe unaotarajia kunufaisha wakazi 7,804.

Mradi huo unaotekelezwa na kampuni ya NT-Business Network kwa gharama ya Sh. bilioni mbili ukiwa na lengo la kuwaondolea wananchi adha ya kutafuta huduma hiyo umbali mrefu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Mkoa wa Njombe (MNEC), Daniel Okoka, wakati wa ziara ya kamati ya siasa ya kutembelea mradi wa maji wa kijiji hicho. Okoka alisema hakuna sababu ya mradi huo kuchelewa kwa maelezo kuwa tayari serikali imetoa fedha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinawafikia wananchi.

"Ni muhimu mkandarasi akaukamilisha mradi huu kwa wakati ili wananchi waanze kuonja matunda ya serikali ambayo imelenga kusaidia wananchi kwa kuwapa huduma stahiki na kwa wakati sahihi," alisema Okoka. Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maji Kijiji cha Mawengi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Ludewa, Isaya Mwita alisema mradi huo ulianza Aprili mwaka 2022.

> **"Ni muhimu mkandarasi akaukamilisha mradi huu kwa wakati ili wananchi waanze kuonja matunda ya serikali ambayo imelenga kusaidia wananchi kwa kuwapa huduma stahiki ...**

Alisema mradi huo unatarajia kukamilika mwishoni Desemba mwaka huu na wananchi wataanza kupata huduma.

Alisema lengo la kukarabati mradi huo ni kuboresha miundombinu ya maji pamoja na kupanua mtandao wa maji ili kufikisha katika maeneo ambayo hayakuwa na huduma ya maji katika vijiji vitatu ambavyo ni Mawengi Lupande na Madunda.

"Mradi huu unatarajia kupeleka huduma hiyo ya maji kwa wakazi wapatao 7,804 na baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi nikiri mkandarasi amekuwa na kasi ndogo jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za serikali," alisema Mwita.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mawengi akiwamo Renato Kahako aliiomba serikali kuongeza usimamizi kwa mkandarasi huyo ili mradi huo ukamilike kwa wakati.



Baadhi ya mafundi wa mkandarasi anayejenga barabara ya njia nne kutoka Nsalaga jijini Mbeya mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wakiendelea kushindilia eneo la karavati, eneo la Mwakapangala Mbalizi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali: Somo la ujasiriamali ni lazima kidato I-IV

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI imesema itakapoanza kutekeleza mtaala mpya wa elimu katika mwaka wa masomo 2027-2028 kila mwanafunzi atasoma madarasa 10 kwa lazima, pamoja na kusoma somo la ujasiriamali kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne ili kukabiliana na tatizo la ajira nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mahongole baada ya kuzindua vyumba sita vya madarasa vya Shule ya Awali na Msingi Magomati iliyopo katika Kijiji cha Usetule ambavyo vimejengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Prof. Mkenda alisema mtaala huo utamtaka kila mtoto wa kitanzania asome madarasa 10 kwa lazima ambapo sita itakuwa ni msingi na minne itakuwa ni sekondari.

"Hatua hii itawawezesha wanafunzi kuwa na uwezo wa kujiajiri hata pale wanapoishia kidato cha nne kwa kuwa watakuwa wanahitimu wakiwa na umri wa miaka 16 tofauti na sasa ambapo wengi wanahitimu elimu ya msingi wakiwa na miaka 13," alisema Prof. Mkenda.

Alifafanua kwamba mtaala huo ukianza kutekelezwa kikamilifu utawawezesha wanafunzi kuanzia kidato cha nne kujifunza masomo ya usajiriamali hasa masomo ya kilimo bora, kushona nguo na michezo.

"Wahitimu watatunukiwa vyeti viwili kimoja cha masomo ya darasani na kingine cha ujuzi kulingana na masomo ambayo amechagua kusoma," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alisema ipo haja ya kujengwa kwa shule ya amari na ufundi mjini Makambako ili kuzalisha wataalamu watakaotumia fursa ya uwepo wa kiwanda cha kuunda magari pamoja na kutengeneza nondo.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Usetule, Christopher Katundu alisema kuzinduliwa kwa shule hiyo kumesaidia kuwapunguzia watoto adha ya kutembea umbali mrefu.

# Ubalozi wa China watoa msaada mitungi, majiko

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan juu ya kampeni ya utunzaji mazingira, ubalozi wa China kwa kushirikiana na kampuni ya Oryx gas wametoa msaada wa mitungi ya gesi 800 pamoja na majiko kwa walimu, madereva, waandishi wa habari na watumishi wa serikali.

Halfa hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania Benoit Arama, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo na viongozi wa dini.

Balozi wa China, Chen Mingjian alisema wanatambua uhusiano mzuri wa kidiplomasia kati ya nchi hizo pamoja na dhamira ya Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan Hassan katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa lengo la kutunza mazingira.

Alisema Serikali ya China inaunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na uoto wa asili.

Chen alisema Tanzania ni nchi rafiki wa mazingira na inazingatia uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Alisema kwa miaka mitatu aliyofanya kazi hapa nchini ameshuhudia juhudi ambazo zimefanywa na Tanzania katika nyanja ya utunzaji wa mazingira.

Alisema mitungi hiyo ya gesi sio tu itaboresha maisha ya walimu bali pia itapanda mbegu za ulinzi wa mazingira katika mioyo ya wanafunzi.

Balozi Chen alisema sera ya China nayo imejikita katika kutunza ukijani, hivyo watashiriki kikamilifu katika kufanikisha malengo hayo, kwamba China itaendelea kushirikiana na Tanzania katika miradi mbalimbali ikiwamo ya nishati safi ya kupikia.

Mkurugenzi Mkuu wa oryx gas Tanzania Ltd, Benoit Araman alisema kuanzia Julai 2021, upatikanaji wa suluhisho la kupika imekuwa mada ya umuhimu mkubwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema programu ya nishati safi ya kupikia itachukua miaka 10 kuwezesha upatikanaji wake kwa ajili ya kupikia kwa angalau asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2034.

Benoit alisema: "Ukizungumza kuhusu nishati safi ya kupikia kwa wanafunzi wenu na katika mikutano na wazazi itachangia kwa kiasi kikubwa kueneza kwa nishati safi ya kupikia nchini Tanzania".

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo alisema oryx gas imekuwa kampuni ya kwanza mkoani Arusha kuonesha dhamira ya kuunga mkono kampeni ya Rais Samia na wamekuwa mstari wa mbele katika kampeni hiyo.

Shekhe wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Arusha, Shaban Juma Abdallah, alisema jamii inapaswa kuhakikisha na kusimamia vizuri misitu ili kutunga mazingira.

Mchungaji Julius Talakwa Laiza aliyewakilisha Askofu wa KKKT Dayosisi Kaskazini Kati, Dk. Godson Abel Mollel, alisema wataendelea kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.



# Wakutana kujadili mchango sekta ya fedha katika uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA wa Shirikisho la Taasisi zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha (TAMFI) wamekutana kujadiliana mchango wa sekta ya fedha katika uchumi na maendeleo ya taifa.

Pia, walijadiliana namna ya kuongeza ufanisi wa huduma ndogo ya fedha ili kuboresha taswira ya sekta ya huduma ndogo za fedha katika jamii.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa TAMFI, Devotha Minzi alisema lengo kuu la kikao hicho ni kutambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha.

Alisema ongezeko la kiasi cha mikopo kinachotolewa na wanachama wa taasisi za huduma ndogo za fedha ni uthibitisho wa uhitaji wa mikopo uliopo nchini.

"Ikumbukwe kuwa taasisi ndogo za fedha zinawakopesha wateja ambao ni hatarishi zaidi kiuchumi na ambao hawana baadhi ya vigezo vya kukopesheka vinavyohitajika na taasisi kubwa za fedha," alisema.

Alisema sekta ya fedha inaendelea kuwa sehemu muhimu sana katika kupanua huduma jumuishi za fedha hasa kwa mikopo inayoenda katika nyanja ya uzalishaji na ujasiriamali.

Devotha alisema miongoni mwa masuala mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na umuhimu wa ufuatiliaji wa miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kuhakikisha kuwa taasisi zote zinazotoa huduma ndogo za fedha zinafuata sheria na taratibu ili kudumisha uwazi na uwajibikaji.

Aidha, Devotha alisisitiza kwamba TAMFI itaendelea kutoa elimu kwa watoa huduma na wateja wao ili kuhakikisha kuwa sekta hiyo inaendelea kukuza uchumi wa jamii na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya kifedha nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMFI, Winnie Terry, alieleza kuwa sekta ya huduma ndogo za fedha ina fursa nyingi sokoni, ingawa bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazozikumba taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha.

Hivyo, alisisitiza kuwa taasisi hizo zina umuhimu katika maendeleo ya taifa, kwamba zinatoa huduma zinazohitajika kwa kiasi kikubwa na wananchi wengi ambao hawapati huduma za kifedha kwa urahisi kupitia mifumo rasmi ya kibenki.

# Waziri ataja mbinu kuongeza wasomi wabobezi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohammed Mussa, amesema ili taifa liwe na wasomi wabobezi lazima taasisi na kampuni ziwekeze katika elimu.

Alisema hayo juzi wakati akizindua programu ya udhamini wa masomo kwa wanafunzi 10 wa Afrika kila mwaka yanayohusiana na teknolojia.

Wanafunzi watakaofaidika na programu hiyo ni kutoka Tanzania, Kenya na Zambia walioanza masomo yao ya shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya data na akili bandia.

Waziri Lela alisema programu hiyo ni ya kwanza katika chuo hicho na ni hatua nzuri iliyofanywa na uongozi wa chuo kwa kutafuta wafadhili ambao watasaidia ufadhili kwa wanafunzi wa Afrika kupata taaluma ya teknolojia.

"Isifike wakati Watanzania hasa Zanzibar tusiwe watazamaji. Ni lazima tuitumie fursa hii kwa sababu imekuja na ipo kwetu katika kampasi hii na mataifa mengine yanakuja kusoma hapa na sisi lazima tupambane ili kunufaika kuwepo kwa taasisi hii ya kimataifa ndani ya Zanzibar," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Tanzania Bara, Omar Kipanga, alisema jukumu la kuelimisha vijana ni la serikali lakini inahitaji kuungwa mkono na wadau wengine wa elimu ili kusonga mbele.

Hivyo, aliwataka wanafunzi kuomba nafasi za mikopo ya elimu ya juu na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zao za kutafuta elimu ili kuhakikisha ndoto na dhamira ya nchi ya kupata wataalamu inafikiwa.

**Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Machano Makame Machano, alisema ufadhili wa wanafunzi hao utainua wigo kwa sekta ya mawasiliano nchini.**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Machano Makame Machano, alisema ufadhili wa wanafunzi hao utainua wigo kwa sekta ya mawasiliano nchini.

Mkurugenzi wa Mawasiliano Airtel, Beatrice Singano, alisema programu hiyo inahusisha wanafunzi wa michepuo ya sayansi hasa katika masuala ya teknolojia.

Alisema, kampuni hiyo kama mdau wa mawasiliano wamechukua nafasi hiyo kuhakikisha wanaingia makubaliano kwa kusomesha vijana kutoka nchi 14 kwa kutoa Sh. bilioni 1.3 kwa mwaka.

Alisema hiyo ni fursa kwa wanafunzi wanaotoka Afrika hasa Tanzania kupata vijana ambao watasaidia kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya teknolojia na mawasiliano.

Wakizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzao waliopata ufadhili huo, Mirium Lukanda kutoka Dar- es salam na Nassir Hemed Nassor kutoka Zanzibar, walisema nafasi hiyo ni ya kipekee kwao kupata taaluma katika chuo cha kimataifa na kuwa wanateknolojia wakubwa duniani.

Masomo hayo yamefadhiliwa na Airtel Afrika Foundation katika Chuo cha IIT Madrass Bweleo.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza na watendaji wa ofisi yake, Migombani, Unguja juzi, wakati wa kikao cha tathmini ya ziara aliyoifanya hivi karibuni katika maeneo mbalimbali kuangalia hali ya mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi ahamasisha uchangiaji fedha afya ya uzazi

**Na Rahma Suleima,**
ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema hatua ya kuchangisha fedha kwa ajili ya afya ya uzazi kupitia kampeni ya 'Uzazi ni Maisha' inayoendeshwa na Shirika la AMREF Tanzania na Wizara ya Afya Zanzibar, itachochea kasi ya maendeleo na mageuzi katika sekta ya afya nchini.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya shukrani na kuchangisha fedha kwa ajili ya afya ya uzazi kupitia kampeni ya 'Uzazi ni Maisha'

Dk. Mwinyi alisema jambo linalotia moyo kuona Zanzibar ipo katika njia sahihi ya kufikia Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Dunia (SDG) ya Mwaka 2030 yanayolenga kupunguza vifo vya wajawazito kufikia chini ya vifo 70 katika kila vizazi hai 100,000.

Alisema kampeni hiyo imekuwa na mafanikio na kwa kipindi cha Juni mwaka huu, AMREF, Wizara ya Afya pamoja na Benki ya ABSA Tanzania wakiungwa mkono na wadau kadhaa walitoa vifaa tiba vya Sh. milioni 262.6 kwa ajili ya vituo vya afya 28 vya mikoa mitano ya Zanzibar.

Aidha, alisema licha ya maendeleo hayo bado kuna changamoto hasa katika kupata rasilimali nyingi kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba.

Hivyo, aliwataka wadau na washirika zaidi kuungana na serikali ili kufikia malengo ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Wakizungumza katika hafla hiyo, wadau hao walipongeza juhudi zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuimarisha afya ya wajawazito na kuahidi kuendelea kuiunga mkono, ili lengo la kupunguza vifo vya mama na watoto lifikiwe.

Mkurugenzi Mkazi wa Amref Health Africa-Tanzania, Dk. Florence Temu, aliwashukuru washirika ambao wamechangia kufanikisha programu hiyo kwa sababu dhamira ya Amref kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar ni kuboresha uzazi salama na afya ya mama na mtoto, sambamba na kupunguza vifo kwa makundi hayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Amref Health Africa - Tanzania, Anthony Chamungwana, alisema Amref Tanzania itaendelea kuwa mshirika thabiti katika ajenda ya huduma za afya kwa wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Obedi Laiser, alisema dhamira ya benki hiyo katika kuboresha huduma za jamii, inajivunia kuunga mkono programu hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF RUNGWE**
**AT TUKUYU**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 22510 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GWANTWA SAIMON KAJUNI**
**AND**
**VUMILIA MWAKANYIKA.........................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made Under rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or Letter of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 9TH day of OCTOBER, 2024.
Dated at Rungwe this 10TH day of SEPTEMBER 2024.

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAJI A. KILIMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha sita chenye Index No. S0485-1081 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAJENGO SECONDARY SCHOOL mwaka 2010, Cheti hiki kimepotea Mkoani KILIMANJARO. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: BNG.RB.4104.2017**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 24110 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HELENA MICHAEL ROBERT**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MUSSA HOSSEINI JUMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of OCTOBER 2024.
Dated at KOROGWE this 26 day of SEPTEMBER, 2024.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 23544 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EDWIN MARTIN NAMPESYA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GLORIA MARTIN NAMPESYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of OCTOBER 2024.
Dated at KOROGWE this 23 day of SEPTEMBER, 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ZUHERY MOHAMED NASSORO**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA WISH YENYE NAMBA ZA USAJILI T 121 DVP. YENYE ENGINE NAMBA 2ZR0553775 NA CHASSIS NAMBA ZGE200051534 KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. AMEFIKA POLISI NA AMEPEWA LOSS REPORT.
TAARIFA POLISI:
**PHQ/TAN/TAN/8051/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVA HANSON KILEO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HILUX YENYE NAMBA ZA USAJILI T453ALA, CHASSIS NAMBA LN1000000688, ENGINE NAMBA 3L2069362. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/TAB/NZE/423/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 234 YA MWAKA 2022**
**SYLVESTER YOHANA MTUMILA (Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Yohana Chigwiye Mtumila ..................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMMANUEL KASUGA NA WENZAKE 2......MJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**EMMANUEL KASUGA**
**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 22.10.2024 saa 3:00 asubuhi.
ANGALIZO: Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03/10/2024.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 24109 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE COTLIDA SIMON NYONI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANANIA MARTIN MAPALA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of OCTOBER 2024.
Dated at KOROGWE this 24 day of SEPTEMBER, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA. Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU Shauri la Madai/Ndoa Na.39/2024 Jina la Mdai: ELISHA MASANJA Jina la Mdaiwa: ADIJA MASANJA BUSUTI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ADIJA MASANJA BUSUTI WA ISANGA, BARIADI**
**KK : VEO ISANGA, BARIADI.**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao(Eleza hapa habari za Madai)Ameleta madai kuwa anadai talaka ili muachane. Kwa hiyo unatakuwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 08 Mwezi 10 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO: Kama hatohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini ,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 Mwezi 9 Mwaka 2024.
Hakimu

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**NYALIKUNGU**

**MKUTANO MKUTANO WASTAAFU KAMPUNI YA SIMU TANZANIA ( TTCL) MWAKA 1994**

MKUTANO WA WASTAAFU WOTE WA KESI YA KUNGUBAYA NA WENZAKE VS KAMPUNI YA SIMU TANZNAIA AMBAYO IPO MAHAKAMA KUU YA JUU (HIGH COURT OF APPEAL) KWA KUSIKILIZWA WARITHI WA MAREHEMUWAJE NA HATI MBALIMBALI ZA MAREHEMU.
MKUTANO UTAFANYIKA MKABALA NA OFISI NDOGO MAKAO MAKUU CCM MTAA WA LUMUMBA JUMAMOSI TAREHE 12 OKTOBA 2024 SAA 4 ASUBUHI.
KWA MAWASILIANO ZAIDI REYNOLD HUNGO

**NAMBA: 0718600422**
**0616234822**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## SAKATA LA GACHAGUA

# Amtwisha zigo Rais Ruto...

## • Adai serikali imejaa ufisadi



Naibu Rais Rigathi Gachagua akizungumza Kirinyaga alipokuwa na Rais William Ruto. PICHA: MAKTABA

**NAIROBI,** Kenya

NAIBU Rais Rigathi Gachagua, amejitetea mbele ya Bunge, kwa kuelekeza mashambulizi makali na ya moja kwa moja dhidi ya Rais William Ruto.

Amedai kwamba, serikali imejaa ufisadi na mauaji ya kiholela ambayo wao wawili, waliahidi kuyakomesha walipokuwa wakifanya kampeni.

Akijitetea dhidi ya hoja 11 zilizokuwa mbele yake, ili asiondolewe mamlakani, alionesha wazi uhusiano kati yake na mkuu wake, Rais Ruto, umeyumba.

Gachagua alitaja mashtaka 11 dhidi yake kama ya kipuuzi na kuwataka wabunge wazingatie sakata la ufisadi, akisema serikalini ndio kumejaa tuhuma hizo.

Juzi, akizungumza na wanahabari kwenye makazi yake rasmi huko Karen, jijini Nairobi, kabla ya kufika katika Bunge la Kitaifa, kujitetea jana, Gachagua aliwashambulia Maspika wa Mabunge mawili; Moses Wetang'ula (Spika wa Bunge la Kitaifa) na Amason Kingi (Spika wa Bunge la Seneti.

Gachagua, amewalaumu maspika hao, ambao aliwalaumu kwa kuwa ni sehemu ya mpango wa umiliki wa hisa za serikali.

"Wananishtumu kwa kuzua mgawanyiko na makabila ninapozungumza kuhusu hisa, ilhali ninaendeleza tu yaliyomo katika mkataba wao wa kabla ya uchaguzi waliotia saini na Rais ambao ulikuwa umefichwa," Gachagua alidai.

Aliwashutumu Wetang'ula na Mkuu wa mawaziri, Musalia Mudavadi, kwa kuweka kipaumbele katika masuala ya eneo lao la Magharibi, huku akimlaumu Kingi, kujadili maslahi yake mwenyewe, ili awe Spika wa Seneti, badala ya kutetea maslahi ya eneo la Pwani anakotoka.

Gachagua anaeleza kwamba hakuwa na maneno mazuri kwa kinara wa upinzani wakati wa uchaguzi, Raila Odinga, ambaye anadai pia ameingia katika mpango wa hisa za serikali.

Alikuwa akirejelea kuundwa kwa Serikali Jumuishi ambayo viongozi wa zamani wa ODM, waliteuliwa mawaziri.

Wanajumuisha waliokuwa naibu viongozi wa chama cha ODM, Hassan Joho na Wycliffe Oparanya; aliyekuwa mwenyekiti wa kitaifa John Mbadi; aliyekuwa Mkurugenzi wa Masuala ya Kisiasa, Opiyo Wandayi na aliyekuwa mwanachama wa bodi ya uchaguzi, Beatrice Askul.

Alisisitiza hakukosea kushambulia hadharani Huduma ya Kitaifa ya Ujasusi (NIS) na maofisa wake wakuu.

Katika mashitaka yaliyomo katika hoja ya kumtimua mamlakani anasema, alijifunza kutoka kwa bosi wake yaani Rais Ruto, ambaye akiwa naibu rais alishambulia idara za usalama.

Juni, mwaka huu, Gachagua alimkosoa Mkurugenzi Mkuu wa NIS, Noordin Haji, kuhusu maandamano ya kupinga serikali nchini, akiilaumu ofisi yake kwa kushindwa kutoa ushauri, kwa kiongozi wa nchi ambao ungezuia ghasia na kuepusha vifo.

**Gachagua, alidai atapambana kuhusu madai ya ufisadi, kudhoofisha serikali na kuchochea chuki za kikabila hadi mwisho.**

Hatua hiyo, ni sehemu ya mashtaka ya utovu wa nidhamu uliokithiri ambayo Mbunge wa Kibwezi Magharibi, Mwengi Mutuse, ameorodhesha katika hoja yake kama msingi wa kuondolewa kwa Gachagua.

"NIS ina jukumu muhimu sana katika kuhakikisha usalama wa nchi yetu. Ina jukumu la kukusanya taarifa za kijasusi na kuzitoa kwa vyombo vyetu vyote vya sheria ili kuhakikisha nchi inakuwa salama wakati wote.

Rais William Ruto wakati mmoja alipokuwa Naibu Rais alimkosoa Mkurugenzi wa Huduma ya Taifa ya Ujasusi wakati huo. Katika video nyingine, alimkosoa vikali Inspekta Jenerali wa Polisi, kwa utendaji kazi duni.

Kwa hiyo nimejifunza kutoka kwa bosi wangu jinsi kazi hii inavyofanywa," anasema.

Anasema kuwa yeye na rais wanakosolewa kila siku lakini hawalalamiki.

Imekuwa ni siku ya kauli kali katika bunge la Kenya huku idadi kubwa ya wabunge wakitoa hoja kali za kuunga mkono hoja kumtimua mamlakani Naibu Rais wa nchi hiyo Rigathi Gachagua.

Mbunge wa Kibwezi Magharibi, Mwengi Mutuse, ambaye aliwasilisha hoja ya kuondolewa mamlakani dhidi ya Gachagua, aliwasilisha kanda za video za Naibu Rais huyo, Februari 2023, alipotoa maoni yake kuhusu serikali kuwa baadhi ya Wakenya ni wenye hisa nyingi na wengine hawana hisa.

Mbunge huyo alisema maoni ya Gachagua yana hatari ya kuigawanya nchi na kuitumbukiza katika siasa mbaya za ukabila.

Mbunge Boss Sholei, Naibu Spika wa Bunge na Mbunge wa Kiti cha wawakili Wanawake wa Jimbo la Uasin Gishu, pia alimshutumu Gachagua kwa uhaini kwa kumhujumu rais katika mikutano yake.

Sholei alianza kwa kujitetea dhidi ya shutuma za upendeleo zilizotolewa na Gachagua ambaye alimshutumu kwa kutumia kiti chake kama Naibu Spika wa Bunge.

"Nataka nithibitishe kuwa sina upendeleo hata kidogo, nilipotoa kauli hizo nilizitoa kama mbunge wa Uasin Gishu na si kwa kama Naibu Spika, unaweza kunituhumu kwa upendeleo tu nikitoa kauli zangu kama Naibu Spika," alisema Sholei.

Sholei, alikariri kauli anazodaiwa kuzitoa Gachagua katika mikutano alizodai zinalenga kuchochea utengano miongoni mwa Wakenya.

Mbunge wa Kaunti ya Likoni Mombasa katika pwani ya Kenya, Mishi Mboko,pia hakutafuna maneno huku akimshutumu Gachagua, kwa kushindwa kutekeleza mkukiuka maadili ya kiapo chake na kuwakosea heshima wanawake.

"Gachagua hana heshima kwa wamama aliita mbunge wetu Malaya," aliongeza mbunge huyo wa Likoni.

### SHUTUMA DHIDI YAKE

Bunge la Kenya, lilijadili hoja 11 kabla ya kumpa naibu wa rais fursa ya kujitetea, na baadaye kupiga kura kuthibitisha hoja moja baada ya nyingine au kuzikataa zote.

Awali, Naibu Rais Gachagua, alifika mbele ya Bunge la Kitaifa, majira ya saa 11 jioni siku ya jana, ili kujitetea dhidi ya mashtaka.

Gachagua, alidai atapambana kuhusu madai ya ufisadi, kudhoofisha serikali na kuchochea chuki za kikabila hadi mwisho.

Kikao maalum kilianza saa tatu asubuhi, jana, mbunge wa Kibwezi Magharibi, Mutuse, alieleza kwa kina mashtaka 11 dhidi ya Gachagua, ambayo anahisi yamevunja sheria na katiba ya Kenya.

Ripoti ya maoni ya Wakenya, kuhusiana na hoja hiyo iliwasilishwa bungeni pia takwimu ya namna walivyopiga kura, zilioneshwa kwa wabunge.

Baada ya kuwasilisha hoja hiyo, mbunge wa Kilifi, Owen Baya, aliunga mkono hoja hiyo.

Bunge, likarejea kwenye kikao cha pili mwendo wa saa nane nusu, asubuhi kwa hoja hiyo kuendelea kujadiliwa hadi atakapowasili Naibu Rais na mawakili wake, kwa kikao maalum cha kujieleza na kujibu maswali ya wabunge.

Kikao hicho cha kamati ya bunge zima, kilisimamiwa na Spika wa Bunge la Kitaifa, Wetangula.

Baada ya saa mbili za kujieleza na kujibu maswali, Gachagua aliondoka bungeni kwa muda.

Usiku wa leo, Spika Wetangula, anatarajiwa kutangaza rasmi kwamba kikao maalum cha bunge kiko tayari kupigia kura hoja hiyo ya kumuondoa kazini, Naibu Rais Gachagua.

Atawaomba viranja wa bunge kupiga kengele ya kuidhinisha kura hiyo kupigwa.

Kura huweza kupigwa kwa njia ya siri kupitia mashine za kompyuta, wanapoketi bungeni.

Kila mbunge ana kadi maalum yenye taarifa zae muhimu ambayo ataitumia kupiga kura, kisha matokeo yatangazwe kwenye Bunge kupitia {screen} iliyopo bungeni.

Ili kupitishwa, wabunge 235 ambao ni theluthi mbili ya wabunge wote nchini Kenya, wanatarajiwa kukubaliana na hoja hiyo.

Ikiwa awamu ya kwanza haitaafikiana na hilo, basi wabunge watarudia kupiga kura.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa Taifa Leo/BBC**

# STRAIKA WA LIGI KUU AONGOZA KWA MABAO CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa timu za Ligi Kuu, Coastal Union na Dodoma Jiji, Raizin Hafidh, anaongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi ya Championship, akifunga mabao manne, katika michezo mitatu ambayo timu yake ya Mtibwa Sugar imecheza.

Raizin, ambaye aliibukia katika Klabu ya Coastal Union miaka mitano iliyopita, msimu huu amesajiliwa na Mtibwa Sugar, yeye na wenzake wakiwa na kazi moja tu ya kuirejea timu hiyo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Straika huyo misimu miwili iliyopita aliichezea Dodoma Jiji kwenye Ligi Kuu, akifunga mabao yote mawili dakika ya 35 na 70 katika mchezo wa kwanza ambapo timu hiyo ilicheza dhidi ya Green Warriors, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Katika mchezo wa pili ambao Mtibwa ilicheza ugenini dhidi ya Cosmopolitan, alifunga bao moja kwenye ushindi wa mabao 2-0, moja likifungwa na Omari Marungu ambaye alipandishwa kwenye kikosi cha kwanza kutoka kile cha vijana chini ya miaka 20.

**Wiki iliyomalizika, straika huyo alipachika tena bao moja katika mchezo mwingine ambao Mtibwa ilicheza nyumbani, Manungu Complex, ikiifunga Mbeya City mabao 2-0, moja likitiwa kwenye kamba na beki wa zamani wa Kagera Sugar, Erick Kyaruzi.**

Hadi kufikia raundi ya tatu ya ligi hiyo, Mtibwa Sugar inaongoza ikiwa na pointi tisa na mabao sita, ikiwa haijaruhusu bao, ikifuatiwa na Songea United ambayo nayo ina pointi tisa na mabao sita, lakini imeruhusu mabao mawili, huku ya tatu ikishikiliwa na Stand United yenye pointi tisa, mabao matatu na haijaruhusu bao.

TMA iko nafasi ya nne na pointi zake saba, Biashara United ikishika nafasi ya tano na pointi zake sita, Geita Gold namba sita, ikiwa na pointi tano. Timu mbili ambazo hazina pointi yoyote wala mabao ya kufunga ni Transit Camp, inayoburuza mkia na Kiluvya FC, inayokamata nafasi ya 15 ya msimamo wa ligi hiyo.



Kamanda wa Polisi Wilaya ya Muheza, Hadija Sokolo (watano kushoto), akiwa pamoja na wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya Jambe Queens baada ya kuibuka na ushindi wa penalti 3-1 dhidi ya timu ya wanawake ya Economy Queens katika fainali ya mashindano ya Ligi ya Polisi Jamii Cup iliyopigwa Uwanja wa Jitegemee, Muheza juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Economy, Jambe Queens Mabingwa Polisi Jamii Cup

**Na Steven William,** MUHEZA

TIMU ya mpira wa miguu ya Wanaume ya Economy FC, kutoka Kata ya Bwembwera wilayani Muheza, Tanga imeibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi FC.

Mchezo huo wa fainali ya michuano ya Polisi Jamii Cup, ulichezwa juzi katika Uwanja wa Jitegemee, Muheza ambapo mgeni rasmi alikuwa Diwani wa Kata ya Majengo, Mukadam Sabuni, akiongozwa na Mratibu wa Mashindano hayo, Koplo Hans Benny Ngollo.

Timu ya Economy FC inayofadhiliwa na Diwani wa Kata ya Bwembwera, Ally Nyangasa, ilipata bao hilo pekee kupitia kwa Kinunga Juma kipindi cha pili.

Kwa upande wa wanawake, timu ya mpira wa miguu ya wanawake ya Jambe Queens iliibuka na ushindi kwa kuifunga timu ya wanawake ya Economy Queens kwa mikwaju ya penalti 3-1 baada ya dakika 90 za mchezo kumalizika kwa sare.

Kutokana na matokeo hayo, Kamanda wa Polisi Wilaya ya Muheza, Hadija Sokolo, alikabidhi zawadi, ambapo mshindi wa kwanza Economy FC, ilizawadiwa jezi seti mbili na mpira mmoja, mshindi wa pili, Polisi FC ilipewa jezi seti moja na mipira miwili huku mshindi wa tatu timu ya Muheza Vetelan nayo ikiondoka na jezi seti moja na mpira mmoja.

Kwa upande wa timu ya Jambe Queens ilizawadiwa seti moja ya jezi na mipira miwili huku timu ya Economy Queens iliyoshika nafasi ya pili ikizawadiwa mipira miwili.

Akizungumza wakati akifunga mashindano hayo, Kamanda wa Polisi Wilaya ya Muheza, Sokolo alisema michezo ni ajira na inasaidia kujenga afya nzuri kwa vijana pamoja na kuwaepusha na tabia mbaya ambazo zinaweza kuwaletea madhara.

Aliwakumbusha wananchi kushiriki katika kujiandikisha katika daftari la makazi huku akiwaomba wananchi kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu katika Jamii.

Kwa upande wa Mkuu wa Kituo cha Polisi Muheza, Kuruthum Bambe, alisema imekuwa ni desturi kwa jeshi hilo kushirikisha jamii katika michezo ambapo alibainisha kuwa dhana hiyo imekuwa na matokeo chanya katika kuwakutanisha jamii na Jeshi la Polisi.

Naye Polisi wa Dawati la Jinsi Wilaya ya Muheza, Inspector Fatuma Mswaki, aliwakumbusha wasichana kutoa taarifa pindi wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia katika michezo na maeneo wanayoishi.

Afisa Utamaduni, Sanaa na Michezo wilaya ya Muheza Msafiri Nyaruva alisema kupitia mashindano mbalimbali ya michezo tayari wameibua vipaji kwa kutoa wachezaji ngazi ya wilaya, mkoa hadi taifa.

# Kocha KMKM aanika siri ya ushindi Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa KMKM SC, Ibrahim Khamis, amesema uzoefu wao katika Ligi Kuu Zanzibar ndio uliowafanya kupata ushindi katika mchezo wao wa tano wa ligi hiyo.

KMKM juzi, Jumatatu walifanikiwa kupata ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya Tekeleza FC kutoka Kisiwani Pemba, mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Nje wa New Amaan Complex.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo msaidizi alikiri timu yake kuzidiwa katika kipindi cha pili cha mchezo hadi kukamilika dakika 90.

Alisema kufanikiwa kupata alama tatu kumetokana na bao lao la mapema walilolipata kabla ya wapinzani wao kuamka.

Alisema wapinzani wao walicheza vema katika eneo la nyuma pamoja na kati jambo lililosababisha kudhibiti mipira ambayo washambuliaji wake walikuwa wakipeleka katika lango lao.

Kocha huyo alisema licha ya wapinzani wao kuwa vizuri katika eneo la ulinzi karibu kipindi chote cha pili, lakini walishindwa kutumia nafasi walizotengeneza.

"Tumepata ushindi, lakini niseme kwa mchezo huu wa leo, uzoefu wa wachezaji wetu wa muda mrefu katika hii Ligi Kuu ndio uliotufanya tupate haya matokeo, mchezo ulikuwa mgumu na wapinzani wetu walikuwa bora sana katika kipindi cha pili," alisema.

Kwa matokeo hayo timu ya KMKM imefikisha alama 10 ikiwa nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo, wakati Tekeleza FC wanaburuza mkia wakiwa na alama moja katika michezo mitano.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TUCHEL ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na Mjerumani Thomas Tuchel mwenye umri wa miaka 51, kama mbadala wa Erik Ten Hag. ***(Manchester Evening News)***

### MARMOUSH AWANIWA LIVER

LIVERPOOOL inavutiwa na mshambuliaji wa Eintacht Frankfurt na Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25. Nottingham Forest na Aston Villa zilitaka kumsajili msimu uliopita. ***(Sky Germany)***

### BEI YA KUDUS KUANIKWA

KLABU ya West Ham inatarajiwa kutoa bei ya kiungo wao wa kati kutoka Ghana Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 24. Liverpool, Arsenal, Manchester City na Chelsea zimeonesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Football Insider)***

### SANE KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapania kumsajili winga wa Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 28, msimu ujao wa majira ya joto, mkataba wake utakapokamilika Bayern Munich. ***(Football Insider)***

### MUSIALA MSHAHARA JUU

BAYERN Munich ipo tayari kumfanya mchezaji wa Ujerumani Jamal Musiala kuwa mchezaji wao anayelipwa kitita kikubwa, pamoja na mshambuliaji wa Uingereza Harry Kane, kwa pauni 400,000 kwa wiki. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 hajadokeza kufanya mazungumzo na Real Madrid au Manchester City. ***(Sky Germany)***

### O'NEIL FRESH KABISA

KLABU ya Wolves wanadumisha uungwaji mkono wao kwa Kocha Mkuu, Gary O'Neil mwenye umri wa miaka 41, baada ya kumfukuza Jack Wilson. ***(Sky Sports)***

### BARCELONA NA DAVID

BARCELONA inamfuatilia mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David, 24. ***(Todofichajes)***

### LARSSON AFUATILIWA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt aliye na umri wa miaka 20 kutoka Sweden, Hugo Larsson. ***(Fabrizio Romano)***

### DIBLING ASHAWISHIWA

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY AWANIWA

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JESUS BADO LULU ARSENAL

**Washikabunduki hao wa London wamekataa kumuuza kwao Brazil licha ya...**

**LONDON,** England

ARSENAL imeripotiwa kukataa mpango wa kumuuza mshambuliaji, Gabriel Jesus kwa Klabu ya Palmeiras ya Brazil.

Jesus alikuwa akianza mara kwa mara baada ya kuhama kutoka Manchester City mwaka 2022, lakini alishuka hadi kwenye benchi baada ya Kai Havertz kusajiliwa miezi 12 baadaye.

**Amecheza mara tano kwenye Ligi Kuu England msimu huu, lakini kwa jumla ya dakika 79 pekee.**

Huku Arsenal ikiaminika kuwinda mshambuliaji mpya, maswali yameulizwa kuhusu mustakabali wa Jesus kwenye Uwanja wa Emirates na waajiri wa zamani, Palmeiras wamedokezwa kujaribu kumtaka mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27.

Katika jimbo la Globo Esporte kulikuwa na mawasiliano kati ya pande hizo mbili katika siku za hivi majuzi wakati Palmeiras ilipotafuta kuungana tena na Jesus, ndipo Arsenal walipomaliza uchunguzi wao haraka.

Kocha Mikel Arteta bado anasemekana kumwona Jesus kama kiungo muhimu wa kikosi chake na hana nia ya kuachana na Mbrazil huyo, ambaye anapigania nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza.

Palmeiras wanadaiwa kukubali msimamo wa Arsenal kwa wakati huu, lakini wanaendelea kuwa na ndoto ya kuungana tena na Jesus, ambaye uhusiano wake wa karibu na klabu hiyo umewafanya waamini kwamba atarejea wakati fulani katika maisha yake ya soka.

## HABARI MICHEZO



# TEN HAG NA MATUMAINI KUBAKI UTD

**MANCHESTER,** England

MUSTAKABALI wa Erik ten Hag kama kocha wa Manchester United unabakia katika usawa kabla ya kikao cha watendaji kilichopangwa wiki hii, ingawa Mholanzi huyo anaamini ataendelea kuaminiwa na wakubwa hao wakati huu wakielekea mapumziko ya mechi za kimataifa, kwa mujibu wa ESPN.

Mmiliki mwenza, Sir Jim Ratcliffe alitazamiwa kuhudhuria mkutano huo uliopangwa mapema mjini London jana Jumanne pamoja na wajumbe wengine wa uongozi wa United, akiwamo mtu wa kulia Sir Dave Brailsford, Mkurugenzi Mtendaji Omar Berrada, Mkurugenzi wa Michezo, Dan Ashworth na Mkurugenzi wa Ufundi, Jason Wilcox.

Familia ya Joel Glazer ambaye inamiliki hisa nyingi, pia ilitarajiwa kuhudhuria.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba maonesho na matokeo msimu huu yamesababisha hofu.

Sare ya bila kufunga na Aston Villa Jumapili iliendeleza mwanzo mbaya zaidi wa msimu wa Ligi Kuu England baada ya kuchukua alama nane pekee kutoka mechi saba za kwanza na kushika nafasi ya 14 kwenye jedwali.

Kwa mujibu wa vyanzo vya habari, Ten Hag alizungumza na timu ya uongozi wa United kutokana na mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Villa Park na hakupewa dalili kwamba kibarua chake kiko hatarini mara moja, hivyo kumfanya aamini kuwa yuko salama kwa sasa.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, sasa ameenda likizo baada ya kuwapa mapumziko wachezaji wa kikosi cha kwanza ambao hawatahusika na michezo ya kimataifa kwa muda wa wiki mbili zijazo.

United watacheza tena dhidi ya Brentford katika Uwanja wa Old Trafford Oktoba 19, mwaka huu.

Kabla ya mkutano wa kamati kuu mjini London siku ya Jumanne, Ratcliffe na Joel Glazer walikutana Old Trafford Jumatatu.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba mazungumzo yalikuwa "ya muda mrefu na ya mikutano mbalimbali."



# Zamalek yajipanga kumsajili Ramos

**CAIRO,** Misri

VIGOGO wa soka Misri, Zamalek hawajafunga kabisa mlango wa kumsajili beki aliyeshinda Kombe la Dunia, Sergio Ramos, licha ya matarajio ya juu ya mshahara wa mchezaji huyo, maofisa wa klabu hiyo wameiambia ESPN.

Ahmed Shawky, mratibu wa vyombo vya habari vya wababe hao wa Misri, amethibitisha kwamba Zamalek wanamtaka mchezaji huyo huru mwenye umri wa miaka 38, lakini amekiri kwamba kuna baadhi ya vikwazo katika kumpa mkataba.

"Baadhi ya mawakala walitoa uwezekano huo," Shawky aliiambia ESPN.

"Bila shaka, Sergio Ramos ni mchezaji mzuri ambaye alishinda kila kitu akiwa na Real Madrid na Hispania. Atakuwa mchezaji mkubwa kwa upande wowote Mashariki ya Kati au Afrika."

Taarifa za Zamalek kutaka kumnunua Ramos, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Sevilla msimu wa majira ya joto, zilitolewa mwezi uliopita, usiku wa kuamkia fainali ya CAF Super Cup ya Zamalek dhidi ya wapinzani wao wa Cairo, Al-Ahly mjini Riyadh Septemba 27, mwaka huu.

"Hakuna kitu kamili hadi sasa, na mchezaji anathaminiwa sana kifedha," Shawky aliendelea, akimaanisha matarajio ya mshahara wa Ramos.

"Pia tunapaswa kukumbuka kwamba Zamalek pia wamesajili mabeki wengine wa kati hivi karibuni.

"Itakuwa msaada mkubwa kwa soka la Misri, na kumaanisha heshima zaidi kwa Zamalek na ligi kama tunaweza kufanya makubaliano."

Uvumi huo uliibua msisimko na shauku miongoni mwa mashabiki wa klabu hiyo, ingawa Hani Shoukry, jumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Zamalek, alidokeza wiki iliyopita kuwa matarajio ya kifedha ya Ramos yangekuwa magumu kwao.

"Kumekuwa na mazungumzo na Ramos ili ajiunge na Zamalek, alifurahia nia hiyo na akakubali kucheza Misri," Shokry aliiambia OnTime Sports.

"Ugumu uko katika masuala ya kifedha na kiasi kilichoombwa na nyota huyo wa Hispania. Ndiyo sababu kuu ya kutokamilisha mpango huo."

# Pochettino aanza kuinoa Marekani

**NEW YORK,** Marekani

MAURICIO Pochettino aliongeza rasmi makocha wake wasaidizi wa muda mrefu kwenye kikosi cha Marekani Jumatatu, siku yake ya kwanza uwanjani kama mbadala wa Gregg Berhalter kuwa kocha mkuu wa timu ya taifa.

Jesus Perez aliteuliwa kuwa kocha msaidizi wa kwanza, Miguel 'Miki' D'Agostino kama kocha msaidizi wa pili, Antonio 'Toni' Jimenez kocha wa makipa na Sebastiano Pochettino - mtoto wake kuwa mwanasayansi wa michezo.

Pochettino alizifundisha Espanyol, Southampton, Tottenham Hotspur, Paris Saint-Germain na Chelsea kabla ya Marekani kumwajiri mwezi uliopita kuelekea Kombe la Dunia la 2026.

Pochettino alisema wakati wa mkutano wake wa utangulizi na waandishi wa habari kwamba alikuwa akiwaleta pamoja na wafanyakazi wake.



Marekani ilianza mazoezi Jumatatu na itacheza mechi za kirafiki dhidi ya Panama Jumamosi huko Austin, Texas na Mexico siku tatu baadaye huko Guadalajara.

Berhalter alitimuliwa Julai baada ya timu hiyo kuondolewa katika raundi ya kwanza kwenye michuano ya Copa America.

## Yanga yajipa nafasi ya robo fainali CAF

INATOKA UK. 24

baadaye tutaona tunakwendaje huko mbele," alisema.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema maandalizi kuelekea kwenye mchezo wa dabi dhidi ya Simba, Oktoba 19, mwaka huu, yameanza rasmi.

Alisema Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ameanza mazoezi na wachezaji waliosalia ambayo hawajaitwa kwenye vikosi vya timu za taifa.

"Timu imeanza kujiandaa na mazoezi kuelekea Oktoba 19 ambapo tutacheza dhidi ya Simba, baadhi ya wachezaji wetu wapo kwenye vikosi vya timu ya taifa, lakini waliobaki wanaendelea na maandalizi.

Ila tunawaombea wachezaji wetu waliokwenda kwenye timu za taifa warejee wakiwa salama bila majeruhi kwani tuna mechi ngumu ya dabi, tunataka kuvuna pointi sita kwenye michezo yetu miwili ya mwezi Oktoba, kwani baada ya hiyo tutacheza dhidi ya JKT Tanzania," alisema Kamwe.

## Morocco: Hakuna wa kuizuia Stars kwenda AFCON

INATOKA UK. 24

lakini na wao hawatokuwa wanyonge kwani wana maelekezo ya kufanya waliyopewa na walimu wao.

"Tumejitahidi kupokea maelekezo ya walimu wetu kuelekea kwenye michezo yetu miwili dhidi ya DR Congo, sisi kama wachezaji tunakwenda kufuata kile tulichoelekezwa kwenye mechi hiyo, tunajua kuwa wenzetu wana wachezaji wazuri sana, wanacheza klabu kubwa nje ya Afrika, hivyo tunajua kama tunakwenda kucheza mchezo mgumu, lakini na sisi tumejiandaa kushinda ugenini," alisema.

Katika mchezo huo, Stars itamkosa mchezaji aliyeitwa kwa mara ya kwanza, Abdulrazack Hamza, ambaye ameumia nyama za paja, ikamlazimu Morocco kumwita beki wa kati wa Mashujaa FC, Ibrahim Ame, kuziba nafasi yake.

Timu hizo zitarudiana tena Oktoba 15 katika mchezo utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mpaka, Dar es Salaam.

Katika Kundi H, Tanzania inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne, nyuma ya DR Congo, yenye pointi sita, Ethiopia ya tatu ikiwa na pointi moja, huku Guinea ikiwa haina pointi na zote zimecheza michezo miwili.

# CHASAMBI AFUNGUKA KUKAA BENCHI SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA chipukizi wa Klabu ya Simba, Ladack Chasambi, amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo akisema kukaa kwake benchi ni kwa sababu ya kujifunza kitu kutoka kwa wakubwa zake, akiahidi siku moja atapata namba ya kudumu, huku akiwakumbusha kuwa hakuna timu yoyote duniani ambayo mchezaji atakwenda na kupata namba kirahisi bila ya kuipambania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Chasambi aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita akitokea Mtibwa Sugar, alisema ni kweli kama binadamu ni lazima ujisikie vibaya kukaa benchi kila mechi, lakini alidai kuwa namba siku zote ni lazima uipambanie na si kupewa kama zawadi.

**Mchezaji huyo amefunguka baada ya mashabiki wengi kulalamika ni kwa nini hapati nafasi ya kucheza, badala yake Kocha Mkuu, Fadlu Davids, amekuwa akimpa zaidi nafasi Joshua Mutale.**

Alisema amekuwa akisikia maneno hayo kutoka kwa mashabiki, lakini yeye binafsi anaona Mutale ni mchezaji mkubwa na mzuri zaidi ambapo yeye mwenyewe ana vitu anajifunza kutoka kwake ndani na nje ya uwanja.

"Ushindani na nafasi ni mkubwa sana Simba, na hapa tu popote kwenye klabu za mpira, haijalishi sijui utoke Simba uende wapi, kote huko, lazima unapoenda ukapiganie namba, wala si vitu vigeni ni vya kawaida tu.

"Nimekuwa nikisikia suala la Mutale, vitu vinaongeleka na navisikia, kwa upande wangu mimi naona Joshua ni mchezaji mzuri sana na mwenye uzoefu mkubwa, anacheza kwa kupambania Simba na ndiyo imemsajili, na hata nikimuungalia siyo kama anacheza vibaya, anacheza vema na mimi nina vitu vya kujifunza kutoka kwake, soka ni nidhamu," alisema Chasambi.

Kuhusu kama anajisikia vibaya kukaa benchi, winga huyo alikiri kuwa kama binadamu ni lazima ajisikie hivyo na hiyo ndiyo itakuwa inamuongezea chachu ya kufanya vizuri zaidi uwanja wa mazoezi ili kumshawishi kocha Fadlu.

"Kama binadamu ni lazima kidogo ujisikie vibaya, lakini kwenye soka ni kawaida, ni lazima upambane ili upate nafasi, umshawishi mwalimu ili kukupa kile ambacho anaona utakileta uwanjani, yaani wala sina hofu na wala mashabiki wasiwe na wasiwasi nitacheza tu, na ikumbukwe wote tunaipambania timu moja," alisema.

Wakati Chasambi akisema hayo, tayari klabu hiyo imemsajili winga mwingine, Elie Mpanzu ambaye ataanza kutumikia timu hiyo katikati ya Desemba mwaka huu.

Usajili wa mchezaji huyo utazidi kuleta ugumu wa namba kwenye kikosi hicho, kwani Mpanzu mbali na kuwa mzoefu wa michezo ya kimataifa, lakini pia ni mmoja wa mawinga wenye uwezo wa kufunga mabao kama mshambuliaji.




Ladack Chasambi

## *Camara, Diarra wachuana kwa 'clean 'sheets'*

**Na Adam Fungamwangwo**

MAGOLIKIPA wawili kutoka Afrika Magharibi, Moussa Camara wa Simba na Djigui Diarra wa Yanga, ni moja kati ya makipa wanne wanaoongoza kwa kusimama langoni mechi nyingi bila kuruhusu wavu wao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Camara, raia wa Guinea na Diarra kutoka nchini Mali, wamefikisha 'clean sheets' nne mpaka sasa katika michezo ya Ligi Kuu ambayo imeingia kwenye raundi ya saba.

Camara amepata 'clean sheets' zake aliposimama langoni kwenye michezo ambayo timu yake ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, mabao 4-0 dhidi ya Fountain Gate, mabao 2-0 dhidi ya Azam FC na bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji. Kwa upande wa Diarra, mechi alizopatia 'clean sheets' ni ile ambayo Yanga ilishinda mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, bao 1-0 dhidi ya KenGold, bao 1-0 dhidi ya KMC na mabao 4-0 dhidi ya Pamba Jiji.

Hata hivyo, Camara amesimama langoni mechi tano, moja akishindwa kulinda 'clean sheets', aliporuhusu mabao mawili, Simba ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union, huku Diarra akidaka mechi nne na zote amefanikiwa kutoruhusu wavu wake uguswe.

Makipa wengine wenye 'clean sheets' nne ambao ni Watanzania ni, Patrick Munthali wa Mashujaa FC na Mussa Mbisa wa Prisons.

Tofauti ni kwamba makipa hawa wakaa langoni mara sita, hivyo wameruhusu wavu wao kuguswa katika michezo miwili ya Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo Nipashe, makipa wenye 'clean sheets' tatu mpaka sasa ni Mohamed Mustafa na Zuberi Foba, wote wa Azam FC, Allan Ngeleka wa Dodoma Jiji, Denis Donis wa JKT Tanzania, Metacha Mnata wa Singida Black Stars, Yona Amosi wa Pamba Jiji na Fabien Mutombora wa KMC.

# Michezo

Jumatano Oktoba 9, 2024

Nipashe




Jesus bado lulu Arsenal UKURASA 21



Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi

## Morocco: Hakuna wa kuizuia Taifa Stars kufuzu AFCON 2025

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kiliondoka nchini jana kwenda Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kucheza mchezo wa tatu wa Kundi H, kwa ajili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, Kaimu Kocha Mkuu, Suleiman Hemed Morocco, amesema wanakwenda kupambana ili kupata ushindi kwani hakuna wa kuwazuia kufuzu fainali hizo.

Akizungumza kabla ya kupaa na ndege maalum ya serikali, iliyotolewa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, Morocco alisema wanafahamu kuwa wanakwenda kucheza mechi ngumu, lakini wamejiandaa kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Stars itajitupa kwenye Uwanja wa Stade des Martys jijini Kinshasa, kucheza na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kesho saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Morocco alisema kwa sasa Stars inaweza kucheza na timu yoyote barani Afrika na kufanya vizuri kutokana na kuwa na wachezaji vijana, wenye uwezo mkubwa wakichanganyika na wazoefu.



"Tunakwenda kucheza na timu nzuri, na wana mwendelezo kwenye ushindi wao, siyo rahisi haitokuwa mechi ya kitoto, lakini naamini na sisi tutakwenda kuleta upinzani ili tushinde mechi hiyo, kama tulishinda dhidi ya Guinea kwao kwa nini tusiifunge DR Congo?

"Kwa sasa timu ya taifa inaweza kucheza na timu yoyote kwa sababu tuna wachezaji wazuri, vijana waliochanga na wazoefu, tunakwenda kupambana kuhakikisha lengo letu mama la kufuzu AFCON linafanikiwa," alisema kocha huyo.

Naye beki wa kushoto wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala' alikiri kuwa wanakwenda kucheza na timu ngumu, yenye wachezaji wengi wanaokipiga nje ya Bara la Afrika,

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yajipa nafasi robo fainali CAF

**Na Adam Fungamwango**

### ● ● ● Yachekelea kundi lao na kueleza ni rahisi kwao huku ikitambia kikosi...

KLABU ya Yanga imesema kutokana na ubora wa kikosi ilichonacho pamoja na uzoefu, itavuka hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kwenda robo fainali kwenye Kundi A lililopangwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Andre Mtine, amesema si kwamba anazidharau timu zingine, lakini anaziona zimo ndani ya uwezo wao, ingawa kwenye soka lolote linaweza kutokea.

**Mtine ameongea hayo siku moja tu baada ya Yanga kupangwa Kundi A la Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwa na timu za TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, MC Alger ya Algeria na Al Hilal ya Sudan.**

Amefafanua kuwa pamoja na ubora ambao timu hizo zinao, lakini si kama Mamelodi Sundowns, Al Ahly, Esperance, Raja Casablanca, Wydad Casablaca, Zamalek na nyingine kubwa na tishio barani Afrika.

"Kwa nilivyoona kundi ni kwamba tunavuka makundi, tuna timu nzuri, ngumu na yenye wachezaji bora wenye viwango na kwa sasa tuna uzoefu pia, pamoja na kwamba si kazi rahisi na si kwamba nazidharau timu zingine, lakini bado zipo ndani ya uwezo wetu, hizi si zile timu tishio barani Afrika ambazo ukipangiwa nazo unaona ni lazima ufanye kazi ya ziada," alisema.

Kwa upande wa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Alex Ngai, yeye amesema haoni kama ni kundi jepesi, lakini matarajio yake ni kuona Yanga ikivuka hatua hiyo.

"Hakuna timu nyepesi kwenye hili kundi, ila sisi mipango yetu ipo vile vile, malengo na matarajio ni kuvuka kwanza hili kundi,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >